# Nipashe Jumapili

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • No. 0581667

Jumapili Mei 5, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


**Waziri** wa zamani wa fedha Mkulo afariki dunia



UKURASA 2

**Takwimu** za mguu kifundo, mgongo kupinda zashtua



UKURASA 4

**Wahalifu** dawa za kulevya wapeana taarifa kutumia sauti ya pikipiki

UKURASA 7



**UNA MIAKA 50? Zingatia haya kutunza mwili**

UKURASA 14

### KIMBUNGA HIDAYA

# Usafiri wa boti na vivuko wasitishwa

UKURASA 2



## Bashe aanika walivyonasa madudu vyama vya ushirika

UKURASA 3



Boti zinazosafirisha abiria kati ya Dar es Salaam na Zanzibar, zikiwa zimetia nanga bandarini Dar es Salaam jana, baada ya kusitisha safari zake, kutokana na upepo mkali unaosababishwa na Kimbunga Hidaya. **Picha ndogo:** Baadhi ya abiria waliofika bandarini hapo kwa ajili ya safari wakitafakari baada ya kurudishiwa nauli zao. **PICHA ZOTE: JUMANNE JUMA**



# Bob Wangwe ajitosa msuguano CHADEMA

UKURASA 3

**MICHEZO** NDUMBARO ANOGESHA BETIKA MBEYA TULIA MARATHON UK.23 **MAONI,** UK.6

# Waziri wa Fedha wa zamani Mkulo afariki dunia Dar

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Fedha wa zamani, Mustafa Mkulo, amefariki dunia katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) akiendelea na matibabu ya maradhi yaliyokuwa yakimkabili.

Kwa mujibu wa taarifa ya mke wake jana, Julie Mkulo, mume wake alifariki dunia juzi hospitalini hapo na shughuli za mazishi zilifanyika siku hiyo Dar es Salaam na anatarajia kuzikwa leo Kilosa mkoani Morogoro.

"Shughuli zote za mazishi zitakuwa msikiti wa Maamur leo (jana) na maziko yatafanyika kesho (leo) Kilosa," alisema.

Mkulo alikuwa Waziri wa Fedha katika Serikali ya Awamu ya Nne na ni mbunge mstaafu wa Kilosa (CCM) aliyetumikia wana Kilosa kwa kipindi cha miaka 10 tangu mwaka 2005 na kutangaza kustaafu wadhifa huo mwaka 2015.

Moja ya sababu ya kustaafu ubunge aliwahi kutaja ni kwa kuwa wakati huo idadi kubwa bungeni ni ya vijana, hivyo kwa umri wake aliona kuwaachia kuchukua nafasi hiyo.

Ni mwenye Shahada ya Uzamili kwenye masuala ya fedha aliyoipata katika Chuo Kikuu cha SouthWest, London, Uingereza kati ya mwaka 1975 na 1977.

Alishika nyadhifa mbalimbali serikalini ikiwamo kuwa Naibu Waziri wa Fedha 2006- 2008 na kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha na baadaye aliengulіwa kutokana na tuhuma mbalimbali zilizokuwa zikimkabili.

Aidha, kwa muda mrefu Mkulo alikuwa Mkurugenzi Mkuu wa uliokuwa Mfuko wa Taifa wa Pensheni kwa Wafanyakazi (NPF) kabla ya kuwa Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF) hadi alipostaafu mwishoni mwa miaka ya 1990 .




Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu (kushoto), wakishiriki katika matembezi ya kilomita 10 ya kuhamasisha ufanyaji wa mazoezi ili kujikinga na magonjwa yasiyo ambukiza, yaliyoanzia Ufukwe wa Coco Oysterbay hadi mzunguko wa Hospitali ya Agha Khan na kurudi Coco Dar es Salaam jana. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, (wapili kulia) ni Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. John Jingu na (kulia) ni Mganga Mkuu wa Serikali, Prof. Tumaini Nagu. Habari Uk. 7. **PICHA: OWM**

KIMBUNGA HIDAYA

# Usafiri wa boti, vivuko wasitishwa

**Na Romana Mallya**

WAKATI vyombo vya usafiri Bahari ya Hindi vikichukua tahadhari kwa kusitisha huduma kutokana na mwenendo wa kimbunga 'Hidaya', Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA), imesema hadi usiku wa kuamkia jana, kilikuwa eneo la bahari takriban kilometa 125 kutoka Pwani ya Kilwa, mkoani Lindi.

Kwa mujibu wa taarifa ya TMA jana, kimbunga hicho kipo kilomita 93 kutoka Pwani ya Mafia na Kilomita 128 kutoka Pwani ya Dar es Salaam, kikiwa na mgandamizo wa hewa wa kiasi cha 985 na kasi ya upepo kilomita 120 kwa saa. TMA ilisema kuwa upepo huo umeendelea kutawala mifumo ya hali ya hewa na kuwa ndani ya saa 6 zilizopita (jana) vipindi vya mvua kubwa na upepo mkali vimeendelea kujitokeza maeneo ya Mtwara, Kilwa, Zanzibar na Dar kuwa na upepo mkali unaozidi kilomita 50.

"Kimbunga Hidaya kinatarajiwa kuendelea kusogea karibu zaidi na ukanda wa Pwani, huku kikipungua nguvu taratibu kuelekea usiku wa kuamkia leo (Jumapili)," ilismea TMA.

Aidha, mamlaka hiyo iliwashauri wananchi wanaojihusisha na shughuli za baharini maeneo yaliyotajwa kuchukua tahadhari kubwa.

Jana, katika fukwe za Bahari ya Hindi Dar es Salaam, shughuli mbalimbali ambazo hufanyika huko, zilikuwa zimesimama zikiwamo boti zinazofanya safari zake Dar es Salaam kwenda Unguja na Pemba.

Baadhi ya abiria ambao walikuwa wamekata tiketi kwa ajili ya kusafiri, walirejeshewa nauli zao kutokana na hali ya hewa kuendelea kuwa mbaya.

Vilevile, wavuvi ambao hujishughulisha na uvuvi katika pwani hiyo walisitisha shughuli hiyo ili vyombo vyao visikumbwe na dhoruba kutokana na kuwapo kwa upepo mkali isivyo kawaida.

Mikoa iliyotajwa na kutakiwa kuchukua tahadhari ya kimbunga hicho kitakachodumu kwa siku tano ni Dar es Salaam, Lindi, Mtwara, Pwani, Morogoro, Tanga na Visiwa vya Unguja.

Tahadhari hiyo imechukuliwa pia, kwa upande wa Zanzibar ambako serikali imesitisha usafiri baharini vinavyotoka Unguja kwenda Dar es Salaam, Pemba na Tanga.

Juzi, Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TEMESA) katika taarifa yake kwa vyombo vya habari, ulisitisha huduma za vivuko katika mikoa mitatu ya Mtwara, Lindi na Pwani baada ya tahadhari kutolewa na TMA.

# Bob Wangwe ajitosa msuguano CHADEMA

**Na Enock Charles**

MKURUGENZI wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA) na kada wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Bob Wangwe, ameshauri na kutoa mbinu katika kumaliza msuguano unaodaiwa kuwamo ndani ya chama hicho.

Amependekeza kuwapo makubaliano baina ya Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe, na Makamu Mwenyekiti wake, Tundu Lissu, kuhusu nani anafaa zaidi kugombea nafasi ya urais mwaka 2025 ili kuepusha misuguano baina ya wanachama.

Katika taarifa yake iliyosambaa katika mitandao ya kijamii jana, Wangwe ambaye ni mwanasheria kitaaluma, alidai kuwa, kwa ushahidi wa kimazingira unaonyesha viongozi hao wawili wamedhamiria kugombea urais mwakani.

Alisema kutokana na hilo, anawashauri wanachama wa chama hicho kutokuwa na upande baina ya viongozi hao, bali kusimama na chama ili kuepusha mivutano.

"Kwa uthibitisho wa kimazingira Freeman Mbowe na Tundu Lissu, wote wamenuia kugombea urais ifikapo 2025, viongozi hawa wawili wana ushawishi na wote wanaweza kugombea na kushinda au kuleta ushindani mkubwa.

"Tukikubali kuchukua upande baina ya viongozi hawa, itamaanisha kuchukua upande wa migawanyiko na kuchafua viongozi wetu, imani yangu ni kwamba, mgombea urais CHADEMA ataamuliwa na Tundu Lissu na Freeman Mbowe wenyewe kabla ya taratibu zingine za chama kuendelea," alisema Wangwe katika taarifa hiyo.

Kada huyo alidai chama hicho kikuu cha upinzani nchini kwa sasa kimekuwa na wanachama wengi kiasi cha watu mbalimbali kutamani kuwania nafasi za uongozi ndani ya chama na zile za kiserikali.

Alisema hatua hiyo imeondokana na utaratibu uliokuwapo miaka ya nyuma wa watu kubembelezwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi.

Kwa mara ya kwanza chama hicho kusimamisha mgombea wa urais tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa ilikuwa ni mwaka 2005 ambao Dk. Jakaya Kikwete (CCM) alishinda na Prof. Ibrahimu Lipumba kushika nafasi ya pili, huku Mbowe akiwa wa nafasi ya tatu kwa matokeo.

Mwaka 2010, CHADEMA kilimsimamisha Dk. Wilbroad Slaa, aliyepata kura zaidi ya milioni mbili sawa na asilimia 26 akishika nafasi ya pili nyuma ya Dk. Kikwete aliyepata kura zaidi ya milioni tano, sawa na asilimia 61, katika uchaguzi uliokuwa na mchuano mkali baina ya CCM na CHADEMA.

Mwaka 2015, chama hicho kilimsimamisha Hayati Edward Lowassa kuwa mgombea urais kupitia UKAWA ukijumuisha vyama vya CHADEMA, CUF, NCCR-Mageuzi na NLD, na kushika nafasi ya pili nyuma ya Hayati Dk. John Magufuli, aliyetangazwa mshindi.

Katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 katika nafasi ya urais, chama hicho kilimsimamisha Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu, aliyechuana vikali na Hayati Magufuli na kushika nafasi ya pili katika uchaguzi uliolalamikiwa na wadau mbalimbali kuwa haukuwa huru na wa haki.

# Bashe aanika walivyonasa madudu ushirika

**Na Vitus Audax,** DODOMA



Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe,

WAZIRI wa Kilimo, Hussein Bashe, aeleza mchezo mchafu unaofanywa na vyama vya ushirika katika minada ya uuzaji wa mazao kwa kufanya udalali katika bei za wanunuzi na kusababisha wakulima kuendelea kuumizwa.

Bashe alieleza hayo juzi bungeni wakati akijibu hoja mbalimbali za wabung, ikiwamo ya kuitaka serikali kuweka bei elekezi ya ununuzi wa mazao hususani mahindi, korosho na kahawa yanayouzwa bei ya chini pamoja na kuuzwa tofauti katika maeneo mbalimbali nchini.

Akijibu hoja hizo, Waziri Bashe alisema si kwamba mazao yanauzwa bei ya chini, bali hali hiyo inasababishwa na watu wachache kuyafanyia udalali na kupata fedha nyingi tofauti na anayopewa mkulima sokoni.

Bashe alisema hujuma hizo kufanywa na vyama vya ushirika na kutaja Katheri akitoa ushahidi bungeni wa karatasi mbili kuwa ni sehemu ya fomu za ununuzi za kampuni ya Harmone Agro Ltd kuwa zinawekwa kwenye debe la mnada na moja ikiandikwa bei na nyingine haina.

Alisema ikifika usiku, ufunguo mmoja anakuwa nao ofisa ushirika na mwingine kiongozi wa ushirika ambao wanaitana na kufungua sanduku na wakishamaliza wanampigia mnunuzi na kumlaghai.

"Wanasema fulani kaandika Sh. 2,000 na wewe umeandika Sh. 1,980 unaonaje uandike Sh. 2,010, alafu sisi utatupa Sh. 30. Kwa hili nina ushahidi, Bunge likiwa tayari nitaweka video ambazo tumerekodi vikao vya siri," alisema huku Bunge likionyeshwa video hiyo ikionyesha watu watatu wakijadili jambo.

"Kinachofanyika kwa kuwa tumeshakubaliana tunaitoa ile karatasi ya bei halali aliyoandika inawekwa bei waliyokubaliana saa nane usiku alafu wanapeana Sh. 30 au Sh. 50," alisema.

Alisema hilo walilibaini kupitia uchunguzi uliofanywa na kamati aliyounda na kufanya kazi kwa kipindi cha miezi mitatu ambapo walikutana na upinzani mkubwa katika ngazi za wilaya.

"Na mimi nilijua kwa kuwa kuna ajali za kisiasa niliwaambia kila mnapofanya mkutano hakikisheni mnarekodi kwa siri na kwa dhahiri, ambapo tulibaini wastani wa fedha iliyochukuliwa na watu wa Katheri ni Sh. 40 hadi Sh. 60, sawa na zaidi ya Sh. bilioni 20 wamegawana," alisema.

Waziri Bashe alisema serikali haiwezi kuruhusu hujuma hiyo na kutoa shukrani kwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe kwa ushirikiano wake wa kuzuia mnada wa ufuta uliotakiwa ufanyike siku tatu zilizopita, ambako walikuwa wamekubaliana debe liwekwe alafu lifunguliwe baada ya siku tatu ili kufanikisha hujuma hizo.

Alisema baada ya kubaini, alimwagiza Mkuu wa Mkoa pamoja na Mkuu wa Wilaya kuzuia kwa kuwa wakulima si wajinga, wanafahamu bei ikishuka na pale inapopanda.

Pia alisema kutokana na hali hiyo walianza mikutano ukiwamo wake na Waziri Mkuu uliofanyika wilayani Karagwe, ambako walikuta kahawa inauzwa kwa Sh. 700 lakini baada ya mkutano huo, inauzwa Sh.3,000.

"Tatizo si mfumo wa ushirika, tatizo ni ili kiongozi wa ushirika aibe ni lazima ofisa ushirika wa wilaya ashiriki kwenye wizi huo, tutazidi kuwabaini wahujumu hao na serikali itaweka mfumo maalumu wa kubaini bei elekezi,"alisema.

Alisema utaratibu huo utaanza na zao la ufuta, mbaazi na korosho na kuwapa haki ya kukataa bei inayoshindaniwa na wanunuzi.

**RIPOTI YA CAG**

Licha ya hujuma hizo, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2022/23 imebaini kuwa Mamlaka 20 za serikali za mitaa hazijakusanya jumla ya Sh. bilioni 5.22 katika chanzo kinachohusu ushuru wa mazao.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, kushindwa kukusanya mapato husika ni kinyume na kifungu cha 7(1) (g) cha Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 inayotaka malipo ya ushuru wa mazao kwa mnunuzi kutozwa asilimia tatu ya bei ya lango la shamba katika mazao ya biashara.

**RC ADAKA VIGOGO**

Waziri Bashe alimshukuru na kumpongeza Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Paul Chacha, kwa kuwakamata na kuwaweka ndani maofisa ushirika watatu wa halmashauri, watendaji pamoja na madiwani wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), kwa tuhuma za kujihusisha na hujuma za aina hiyo katika zao la tumbaku. Alisema watu hao walikamatwa kwa kufanya ukangomba (hujuma) katika zao hilo na kudai kuwa, amebaki Mstahiki Meya wa Manispaa ya Tabora ambaye alidai kuwa, aliiba mbolea za wakulima na sasa yupo mtaani.

Alisema Meya huyo hana kinga ya kushtakiwa na kuagiza yeyote atayehujumu juhudi za serikali, achukuliwe hatua stahiki bila kujali wadhifa wake, wala ukaribu wake na kiongozi yeyote.

"Niwape moyo wakuu wa mikoa pamoja na wakuu wa wilaya, kuwa yeyote anayehujumu shughuli na miradi ya wakulima katika ngazi ya Wilaya nchini mna mamlaka mliyopewa na Rais, itumieni maana hatutaruhusu nguvu zinazopelekwa na serikali alafu watu wachache wakafaidike na jasho la wakulima," alisema.

**UTITIRI TOZO**

Waziri Bashe alitumia Bunge hilo kupiga marufuku utitiri wa tozo kwa wakulima tofauti na zile zilizowekwa kwa mujibu wa sheria zikiwamo tozo za Sh. 20 kwa kata,20 kwa wilaya pamoja na Sh. 10 kwa mkoa, na kuwa tozo zitakazobaki ni zile zinazotambuliwa na serikali.

"Fedha hizo zote ukipiga hesabu kwa tani 300,000 ni sawa na Sh. bilioni 50 mkulima anachukuliwa, hivyo halmashauri ikishachukua ushuru wake unatosha,"alisisitiza.

Alisema fedha hizo zilikuwa zinakatwa kwa madai ya ujenzi wa maeneo husika na kueleza kuwa kwa sasa serikali inapeleka fedha moja kwa moja katika maeneo husika, hivyo hakuna haja ya kuwanyonya wakuli.

Vilevile alisema serikali itapunga Sh. 10 kutoka kwenye tozo ya bodi ya korosho na Sh.10 kwenye tozo ya tari ,ili kuondoa mzigo mkubwa kwa wakulima.

# Takwimu mguu kifundo, mgongo kupinda zashtua

**Na Romana Mallya**

TAKWIMU za watoto wanaozaliwa na mguu kifundo, mgongo kupinda na mtindio wa ubongo ambao wengi hupokewa katika Taasisi ya Tiba ya Mifupa na Ubongo Muhimbili (MOI) wakiwa wamecheleweshwa, imeshtua na kuanza kuwasaka mitaani.

Kwa mujibu wa wataalam, ucheleweshaji huo husababisha mtoto kufanyiwa upasuaji ambao hubaki na maumivu maisha yake yote, wakati angewahishwa angepona.

Meneja wa Kitengo cha Upasuaji Mifupa na Viungo Watoto MOI, Dk. Bryson Mcharo, ambaye ni Bingwa Mbobezi Upasuaji Mifupa na Viungo Watoto, aliyasema hayo kupitia mahojiano maalum na mwandishi wa habari hizi yaliyofanyika Alhamisi, wiki hii.

Dk. Mcharo alisema kutokana na ongezeko hilo, MOI imeanza kuwasaka mtaani kupitia programu maalum iliyoanza Mei Mosi, mwaka huu, kwa kuendesha huduma ya tiba ya mifupa na viungo kwa watoto mikoa mbalimbali.

Alisema wameamua kufanya hivyo kwa kuwa, kati ya watoto wanaofikishwa hospitalini hapo, baadhi huangukia kwenye upasuaji kutokana na kucheleweshwa.

Alisema taasisi hiyo ina kliniki tatu kwa wiki zinazofanyika siku za Jumatatu, Jumatano na Alhamis ambapo Jumatano imetengwa kwa ajili ya miguu kifundo na hupokea watoto kati ya 10 hadi 30.

"Siku ya Jumatatu tunapokea kati ya 80 hadi 100 na wengi wao ni wale wanaendelea na kliniki, wapya huwa kati ya 10 hadi 15. Mtoto anapowahishwa hospitalini mapema anaweza kuchukua takribani wiki nne hadi sita hadi kufikia kuvalishwa kiatu. Na kuwahi inasaidia mguu kutibika.

"Changamoto huja mtoto anapocheleweshwa hospitalini itabidi upasuaji na atakuwa na kovu, kunyoosha mifupa ambapo hatua hizi zinaweza kukuletea maumivu baadaye. Unaweza kutibu ulemavu, lakini ukabaki na tatizo la maumivu maisha yote," alisema.

Dk. Mcharo alisema changamoto nyingine ambayo atakutana nayo ni unyanyapaa mpaka miaka 10 hadi 20 na kuleta shida ya kisaikolojia kwa mhusika.

Alibainisha kuwa, watoto wanaowapokea kwenye kliniki hospitalini hapo ni mpaka umri wa miaka 16, kwa kuwa wasichana wanakoma kukua mifupa yao mpaka miaka 14 na wavulana mpaka miaka 16 wanaendelea kukua.

Dk. Mcharo alisema waliandaa programu ya kuwafikia watoto hospitalini hapo siku ya Mei Mosi iliyokutanisha watoto na madaktari bingwa wa mifupa, ambayo lengo lake lilikuwa ni kuwaona watoto kati ya 100 hadi 200, lakini waliofika wagonjwa wapya watoto 126.

Alisema waliamua kuendesha programu hiyo kwa kuwa, MOI imekuwa ikiendelea kuwapokea watoto hao wakiwa wamecheleshwa matibabu.

"Wangekuja mapema, wangepata matibabu kwa gharama rahisi kwao, kwa taasisi na serikali kwa ujumla, lakini kwa sababu zilizo nje ambazo hatujazijua, kumekuwa na ucheleweshaji wa watoto kufika hospitalini.

"Wengi wanakuja wamechelewa, ama wamepata matibabu ambayo si sahihi huko. Kama idara tumeona tutoe elimu na kufanya kliniki ambapo pamoja na kuwasaidia, huduma itawafikia watanzania wengi ili wawalete watoto hospitalini mapema," alisema.

Dk. Mcharo alisema wengi wao waliowahudumia siku ya Mei Mosi, ni wale waliokuwa nyumbani ambao hawajawahi kutibiwa matatizo yao.

Alisema miongoni mwao wapo wenye matatizo ya mguu kifundo, wenye utindio wa ubongo unaopelekea kupata matatizo ya nyonga, mifupa ambao walikuwa wengi.

"Tunapoongelea matatizo ya mifupa kwa watoto wadogo, huanzia pale mtoto anapozaliwa, kuna uwezekano wa watoto kuzaliwa nayo, mfano mguu kifundo, takwimu zinaonyesha katika watoto wanaozaliwa 750 mpaka 1,000.

"Tukichukuliwa idadi ya watu kwa Tanzania, tunaweza kuona kwa namna gani kuna watoto wangapi waliozaliwa na matatizo haya takwimu zinaonyesha ni asilimia moja mpaka tano ya watanzania wote.

"Kwa hiyo tuna zaidi ya watu 600 wako mahali na inawezekana hawajatibiwa kabisa kwa kuwa, tunapata watoto ambao hawajawahi kutibiwa na migongo imepinda upande," alisema.




Meneja wa Kitengo cha Upasuaji Mifupa na Viungo Watoto MOI, Dk. Bryson Mcharo, ambaye ni Bingwa Mbobezi Upasuaji Mifupa na Viungo Watoto, akizungumza na mmoja wa wazazi wa watoto waliohudhuria kliniki ya matatizo ya mifupa na viungo, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. **PICHA: ROMANA MALLYA**

**NINI CHANZO?**

Dk. Mcharo alisema yako matatizo ambayo mtoto hupata wakati wa ukuaji wake, kama upungufu wa lishe au Vitamin D inayosababisha kupata matege.

Pia alitaja kundi lingine la ukuaji wa mtoto ambao haushabiani kati ya upande wa ndani wa mfupa na nje na kusababisha kupinda miguu.

Alisema wWatoto wa aina hiyo ni wengi kwa kuwa, wakiangalia takwimu zilizowahi kutolewa duniani, wanaona kuna watoto wengi wanazaliwa na matatizo hayo.

"WaKo wanaopata wakati wa ukuaji, tunapoongelea maambukizi katika mfupa , maungio hawa watoto wapo wengi sana.

"Tumeona si busara kukaa na kupokea watoto ambao wanafikishwa hapa wakiwa wamecheleweshwa. Tukiangalia mifumo ya nchi nyingine wamekuwa wakiendesha hizi programu kwa kutoka nje ya taasisi na kuwapata watoto mapema na wananchi nao wanapata elimu ya kuwawahisha hospitalini mapema," alisema.

Mtaalam huyo alisema wameanza programu hiyo Mei Mosi na kwa Mkoa wa Dar es Salaam, wataendelea Mbagala, Gongo la Mboto, Tegeta na baada ya hapo watazunguka nchi nzima ikiwamo mikoa ya Morogoro na Tanga.

Alisema waKo watoto ambao hupokewa MOI kupitia taasisi zisizo za kiserikali ambao wengi wao huwa hupatikana mitaani wakiwa wamezidiwa na hawajiwezi.

"Hata jamii inawaona, lakini inashindwa kujua iwapelekea wapi, tunafikiri kupitia programu hii tutafikia watanzania wengi. Tunaomba watanzania watuunge mkono ili kuzuia ulemavu wa aina hii unaotibika," alisema.

HABARI KITAIFA

# Mbaroni madai kulaghai watu kazi

Na Romana Mallya

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam linawashikilia watuhumiwa 10 akiwamo raia wa Kenya kwa tuhuma mbalimbali zikiwamo kujifanya wakala wa mafunzo ya biashara na kujipatia fedha na anayetumia picha za viongozi kuwalaghai watanzania atawapatia kazi na uhamisho.

Kamanda wa Kanda hiyo, Kamishna Msaidizi mwandamizi (SACP) Jumanne Muliro, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu operesheni maalum iliyoanza mwezi uliopita. Alisema katika operesheni hiyo, walimkamata, Hassan Chambilia Sumilanda (28) maarufu Dk. Hassan Mangena, mkazi Sinza Kumekucha, anayetumia picha za viongozi wakuu serikalini kuwalaghai watanzania kuwa atawasaidia kupata kazi na uhamisho.

Alisema mtuhumiwa huyo anatuhumiwa kufanya hivyo ili kujipatia fedha kwa njia ya udangayifu kwa kudai kuwasaidia watu kupata kazi au uhamisho jambo ambalo siyo la kweli.

"Mtuhumiwa huyu amekuwa akitumia fursa mbalimbali za hafla za kiserikali kupiga picha na viongozi wakubwa wa serikalini na kuziweka katika kurasa mbalimbali za mitandao ya kijamii kwa jina la Hassani Mangena na kujitambulisha kuwa ni mtumishi wa serikali kutoka Wizara ya Afya, Kitengo cha Mama na Mtoto.

"Wakati mwingine hujitambulisha kuwa ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu," alisema.

Kamanda Muliro alisema wanawahoji watuhumiwa wengine wanne ambao ni Javani Ochengi (36), raia wa Kenya, anayeishi Kimara, Yohana Mroso (20), mkazi wa Mbagala, Fransis Asangwile (34), mkazi wa Kongowe na Auston Mpanju (32), mkazi wa Tuangoma, wanatuhumiwa kujipatia fedha kwa udanganyifu.

Alisema watuhumiwa hao wamekuwa wakijinadi kuwa wao ni wakala wa mafunzo ya biashara na kwamba, watawatafutia vijana shule, vyuo, kazi au sehemu za utalii nje ya nchi.

"Watuhumiwa hao wamekuwa wakitumia kampuni ijulikanayo kwa jina la PROFFESION EXCHANGE PLATFORM (PEXPLA) kuwahadaa watu walipe fedha ili wasaidie kupata nafasi wanazohitaji, kitendo kilichowezesha kukusanya kiasi kikubwa cha fedha kutoka kwa wananchi kisha kutoweka," alisema.

Kamanda Muliro pia, alisema wanamshukilia, Essau Fransis (27), maarufu Makumba mkazi wa Makumbusho na wenzake wanne wakiwa na luninga 35 zilizoibwa katika maeneo mbalimbali Dar es Salaam na sita kati yake zimeshatambuliwa.

Alisema Jeshi la Polisi linatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa taarifa za kweli na linaahidi kuzitunza kwa siri na halitakuwa na huruma kwa mtuhumiwa yeyote anayejihusisha na vitendo vya kihalifu.



Kamanda wa Polisi Kanda Maalumu ya Dar es Salaam, SACP Jumanne Murilo akionyesha televisheni 35 kwa waandishi wa habari, jijini humo jana, zilizokuwa zimeibwa katika maeneo mbalimbali baada ya kuzikamata katika operesheni inayoendelea ambapo watuhumiwa watano wametiwa mbaroni. Aidha amewataka wananchi kuchukua tahadhari kwa mabadiliko ya hali ya hewa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Mwananchi amzawadia 5,000/- Rais Samia

Na Munir Shemweta, MLELE

MKAZI wa kijiji cha Luchima katika kata ya Majimoto, Halmashauri ya Mpimbwe, Mlele mkoani Katavi, Aseni Jandikile, amemzawadia Sh. 5,000 Rais Samia Suluhu Hassan kwa kile alichosema ni kutokana na juhudi zake za kuwaletea maendeleo wananchi.

Kiasi hicho cha pesa alikikabidhi juzi kwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ambaye ni Mbunge wa Kavuu, wakati akizungumza na wananchi wa kijiji cha Luchima wakati wa ziara yake ya kuwafariji wananchi waliopatwa na mafuriko katika jimbo hilo.

"Nampongeza Rais kwa vitendo kabisa. Naomba Mheshimiwa Mbunge nikukabidhi fedha taslimu Sh. elfu tano umpelekee Mheshimiwa Rais, " alisema.

Kwa mujibu wa mwananchi huyo, uamuzi wake unatokana na kuvutiwa na uongozi bora na utendaji kazi wa Rais Samia hasa kwa kuwajali wananchi wa Luchima. Alisema pamoja na mambo mengine, amewajali kwa kutoa Sh. milioni 50 kwa ajili ya ujenzi wa zahanati ambayo alisema imewakomboa wananchi wa kijiji hicho.

Naibu Waziri Pinda alisema fedha hizo zilizotolewa na mwananchi huyo, zitamfikia Rais Samia.

Pinda alimpongeza mwananchi huyo kwa uamuzi wake wa kutoa kiasi hicho cha fedha kama ishara ya kukubali juhudi na kazi kubwa inayofanywa na Rais Samia katika kuwaletea maendeleo wananchi wa Luchima na Tanzania kwa ujumla.

Aluiwaeleza wananchi wa kijiji hicho kuwa Rais Samia anawapenda na amekuwa akisaidia juhudi mbalimbali za maendeleo kwenye jimbo la Kavuu na kutaja baadhi ya juhudi hizo kuwa ni pamoja na kutoa fedha za ujenzi wa hospitali, shule, barabara pamoja na upatikanaji wa huduma za maji. Pinda alifanya ziara katika jimbo la Kavuu kuwafariji wananchi waliopatwa na mafuriko yaliyosababishwa na mvua kubwa iliyoathiri pia miundiombinu yakiwamo madaraja.

# Biteko apongeza mchango kanisa kwa maendeleo

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko, amepongeza mchango wa kanisa katika maendeleo ya jamii na kuwashauri wachungaji kuwa na maono makubwa katika kuongoza waumini ili kujenga taifa la watu wenye mwelekeo chanya.

Biteko alisema hayo juzi jijini Dodoma wakati wa kufunga kikao cha mazungativu (Retreat) kwa wachungaji wa Kanisa la FPCT.

Alisema ili waumini wapate uelekeo wa kwenda mahali fulani, wanahitaji mtu mmoja miongoni mwao atakayewaongoza kufikia malengo waliyojiwekea kutokana na maono aliyo nayo.

"Wachungaji msihangaike na wingi wa watu mahali popote. Angalia uwezo wa kiongozi anayeona mbali atawaongoza wafike mbali.

"Askofu Mkuu umechagua fungu jema kufanya wachungaji hawa wakutane hapa kujiongezea maarifa kwa kuwa tuko katika dunia iliyojaa utandawazi na mafundisho ya kweli na yasiyo ya kweli. Ni vigumu kwa waumini kutambua ya kweli na yasiyo ya kweli hivyo, wanahitaji kuongozwa," alisema.

Aidha, Dk. Biteko amewahimiza viongozi wa dini kuwaongoza waumini kiroho na kuchagua viongozi sahihi wanaofahamu kuwa watawaletea maendeleo na ustawi wa nchi.

Pia aliwaomba viongozi wa dini kuwahimiza waumini kufanya kazi kwa bidii, kuhubiri kuhusu amani pamoja na kusisitiza maadili kwa waumini.

Dk. Biteko alitaja mafanikio mbalimbali ya serikali huku akiwaomba wachungaji hao kuendelea kumuombea na kumtia moyo ili aendelee kutekeleza miradi ya nchi katika maeneo mbalimbali.

" Mradi wa reli ya kisasa (SGR) ni mkubwa. Haikuwa rahisi kupata fedha za kutekeleza mradi huu lakini Rais Samia Suluhu hassan amefanikiwa. Mradi wa ujenzi wa Bwawa la Julius Nyerere unaozalisha megawati 2,115 umefanikiwa. Pia serikali imejenga madarasa, zahanati, vituo vya afya na kutoa ajira kwa watumishi wa sekta ya afya, angalieni nia yake, muungeni mkono," alisema.

Pia alisema serikali inatambua umuhimu wa dini na imani za watu hivyo viongozi wa dini wahimize waumini kuchagua viongozi wanaofaa.

"Mwaka huu tuna uchaguzi wa serikali za mitaa. Viongozi wa dini mna uwezo wa kuwahamasisha waumini waweze kuchagua viongozi wanaowahitaji kwa ajili ya kuwaletea maendeleo," alisisitiza.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Watanzania washiriki mazoezi ili kuepuka magonjwa yasiyoambukiza

**WAZIRI** Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alishiriki mazoezi ya pamoja ya kampeni ya kitaifa inayoratibiwa na Wizara ya Afya ya kuhamasisha Watanzania kufanya mazoezi ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza kama vile shinikizo la damu, maradhi ya moyo na kisukari.

Katika ushiriki wake huo, Majaliwa alisema hatua hiyo pia ni kuunga mkono wito wa Rais Samia Suluhu Hassan wa kufanya mazoezi ili kujikinga na magonjwa hayo. Kutokana na kasi ya kufanya mazoezi na kuandaliwa eneo maalumu la Coco Beach, Dar es Salaam kwa ajili ya jambo hilo, Waziri mkuu alilitaka Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi wa eneo hilo ili liendelee kuwa salama.

Programu ya ufanyaji mazoezi ilianzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan na yeye mwenyewe kushiriki na kuwahamasisha watanzania kushiriki mazoezi mbalimbali, huku akisema moja ya mambo ya kujivunia katika kipindi chake cha miaka mitatu ya uogozi ni mafanikio katika sekta ya michezo.

Wakati hayo yakifanyika, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alibainisha kuwa kutokana na ongezeko la magonjwa 10 yasiyo ya kuambukiza wizara ilileta ombi la kuanzisha utaratibu huo kila Jumamosi.

Waziri Ummy alibainisha kuwa mwaka 2022, kati ya magonjwa 10 yanayowasumbua Watanzania, moja lililojitokeza ni shinikizo la juu la damu likifuatiwa na kisukari, hivyo kuona kuwa njia mojawapo ya kudhibiti na kupunguza tatizo hilo linalokua kwa kasi ni kuanzisha mpango wa mazoezi.

Wito wa kufanya mazoezi hivi sasa umekuwa kama wingo usio na mwisho kwani viongozi wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa kufanya hivyo ili kupunguza uwezekano wa wananchi kupata maradhi yasiyo ya kuambukiza ambayo kwa kiasi kikubwa yanatokana na mtindo wa maisha. Watu wamekuwa hawafanyi mazoezi au kushiriki michezo hatua ambayo inachochea kuongezeka kwa maradhi hayo.


Mtu anaweza, kwa mfano, akatoka ndani ya nyumba na kuingia kwenye gari na kwenda moja kwa moja ofisini na wakati anapoamka hafanyi hata mazoezi au kutembea hatua kadhaa kuupa mwili wake nishati. Akifika kazini, anakaa ofisini mpaka muda wa kumaliza kazi na baadaye kuingia kwenye gari moja kwa moja nyumbani. Hata akifika nyumbani, anakaa na kuangalia televisheni kisha kula na kwenda kulala.

Hata katika shule, hivi sasa hakuna mchakamchaka katika shule nyingi na hata mazoezi yanaonekana ni adhabu kwa wanafunzi. Hata hivyo, serikali inastahili pongezi kwa hivi karibuni kutamka kuwa mchakamchaka ni lazima katika shule zote, ziwe za binafsi au za umma ili kuwaweka katika hali njema kiafya na kuwaepusha dhidi ya maradhi yasiyo ya kuambukiza.

Kwa hakika, magonjwa yasiyo ya kuambukiza ni janga linalolinyemelea taifa kutokana na takwimu zinazotolewa mara kwa mara juu ya kuendelea kuongezeka. Kutokana na ukweli huo, suala la mazoezi kwa wananchi wote linapaswa kupewa uzito unaostahili.

Tunasema hivyo kwa sababu taarifa katika taasisi za afya kama vile hospitali zinaonyesha kuwa magonjwa ya moyo, shinikizo la damu na kisukari yanazidi kuongezeka huku sababu kubwa zikitajwa kuwa ni mtindo wa maisha wa watu kutokufanya shughuli za kuwafanya watoke jasho kama vile mazoezi na ulaji wa vyakula na unywaji wa pombe kupita kiasi.

Ni vyema sasa Watanzania wakazingatia maonyo na mashauri ya viongozi na wataalamu wa afya kwa kuzingatia masharti katika ulaji na unywaji wa vileo. Kwa kufanya hivyo, ni dhahiri kwamba maradhi mengi, hasa yasiyo ya kuambukiza yatapungua na hatimaye fedha nyingi zinazoelekezwa kwenye matibabu, kupelekwa kwenye miradi ya maendeleo.




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kasi ya kuelimisha vijana fursa zilizopo iongezeke



Na Sabato Kasika

**HIVI** karibuni, awamu ya pili ya mradi wa kuwalinda vijana uitwao Safegurd Yiung People (SYP), ulizinduliwa na Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, Patrobas Katambi.

Mradi huo unaendeshwa kwa ushirikiano, kati ya Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, ubalozi wa Uswiss nchini na serikali ya Tanzzania.

Katika uzinduzi huo, Waziri Katambi anasema serikali ya awamu ya sita imeyapa kipaumbele masuala ya maendeleo ya vijana, na kwamba wao kundi muhimu katika taifa, kwa ajili ya kuleta maendeleo.

Ninaunga mkono vijana kupewa kipaumbele katika harakati za kujiletea maendeleo au kuleta maendeleo kwa taifa lao, kwa kutambua kuwa wao ndio nguvu kazi ya taifa na idadi yao ni kubwa.

Akikariri matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, Katambi anasema, vijana nwalifikia milioni 21.3 sawa na asilimia 34.5 ya watu wote, vijana wa kiumeb ni milioni 10.1, wa kike ni milioni 11.1.

Lakini pia anakariri Utafiti wa Nguvu Kazi, 2021 (ILFS, 2021), kwamba, Tanzania ina nguvu kazi ya watu milioni 25.8. Kati ya nguvu kazi hiyo, vijana ni milioni 14.2 sawa na asilimia 55.6.

Kwa msingi huo, ni wazi vijana ni injini ya maendeleo ya taifa, hivyo ninadhani serikali haina bndi kuchukua hatu mbalimbali za kuwawezesha ili wawe na manufaa kwa katika jamii na taifa kwa ujumla.

Katika idadi hiyo, ninaamini wapo vijana ambao wanarandaranda mitaani, kushinda vijiweni na wengine kushinda katika vituo vya mabasi wakipiga debe ili kujikimu kimaisha.

Vilevile, wapo ambao wamejiajiri au kuajiriwa na wengine kuzunguka na vyeti vya taaluma, katika ofisi za umma, binafsi na katika mashirika kutafuta ajira na wengine kutafuta mikopo ili kufanya biashara.

Ninatambua juhudi zinazofanywa na serikali za kuwawezesha vijana walio katika sekta isiyo rasmi na wahitimu wa vyuo kuweza kujiajiri kwa kuanzisha miradi mbalimbali ya uzalishaji mali hasa kilimo.

Lengo ni kutaka wapate mitaji, kwa kuboresha Mwongozo wa Utoaji Mikopo kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Vijana (YDF) na sasa mbali na kutoa mikopo kwa vikundi vya vijana na kampuni, mfuko huo sasa unatoa mikopo kwa kijana mmoja mmoja.

Hivyo, wakati ikiliangalia kundi la vijana wasomi, ni vyema pia wanaoshinda katika maeneo nilioyataja awali, nao wakatafutiwa njia za kusaidiwa ili wawe na hali inayoakisi maisha bora ya baadaye.

Kwa mujibu wa naibu waziri huyo, mwaka huu wa fedha Mfuko wa Maendeleo ya Vijana, umetoa mikopo yenye thamani ya Sh. 1,274,471,500 kwa miradi ya vijana 56 yenye wanufaika 392.

Lakini pia anabainisha kuwa kuna mifuko mingine ya uwezeshaji wananchi kiuchumi ambayo kwa ujumla wake inaratibiwa na Baraza la Taifa la uwezeshaji wanachi kiuchumi (NEEC).

Hapa anataka vijana waifahamu na kutumia fursa hizo kujikwamua kiuchumi. Hatua zinazochukuliwa na serikali kwa ajili ya vijana ni nzuri, lakini sidhani kwamba wengi wao wanazijua fursa hizo.

Inalezwa kuwa kua programu ya taifa ya kukuza ujuzi ambayo imewawezesha vijana 133,448 kupata mafunzo ya kukuza ujuzi katika fani mbalimbali, huku vijana 78,598 wakiwa wamepatiwa ujuzi na stadi mbalimbali za kazi kupitia mafunzo ya uanagenzi.

Katika programu hiyo, inaelezwa na naibu waziri kuwa vijana 20,334 wamepatiwa mafunzo na kurasimishwa ujuzi walioupata nje ya mfumo rasmi wa mafunzo na kupatiwa vyeti ili wavitumie kutafuta ajira, kujiajiri na kujiendeleza kiujuzi katika taasisi mbalimbali za mafunzo.

Kimsingi hatua hizo zote ni nzuri kwani zinalenga kuwainua vijana ambao ni nguvu kazi ya taifa, lakini ninaamini ninadhani serikali bado ina safari ndefu, kutokana na kwamba kundi kubwa bado halijafikiwa.

Hivyo, ingekuwa vyema kuongeza kasi ya kuwaibua na kuwaisadia lakini vijana hasa wanaoshinda vijiweni wangekuwa wanafuatilia taarifa mbalimbali zinazowahusu ili wajue nini kinaendelea kuhusu wao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

SAFU

## FIKRA MBADALA

# Hakuna uhuru wa Habari bila uchumi wa vyombo vya habari



Pascal Mayalla

WIKI hii nzima nimekuwa jijini Dodoma kuhudhuria mikutano mitatu muhimu ya mambo ya habari. Tulianza na Mkutano Mkuu wa 13 wa Mwaka wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), uliojikita kwenye kuhamasisha matumizi ya gesi ili kunusuru mazingira kwa ukataji miti ya kuni, na kuchoma mkaa. Mgeni rasmi alikuwa Naibu Waziri Mkuu na Waziri wa Nishati, Dk. Doto Biteko.

Baada ya hapo, ukaja Mkutano wa Baraza la Habari Tanzania, uliozungumzia nafasi ya vyombo vya habari katika uchaguzi mbalimbali, mgeni rasmi akiwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, Jaji Joseph Warioba, na Ijumaa tukaadhimisha Siku ya Kimataifa ya Uhuru wa Habari, kuzungumzia uhuru wa Habari. Hapo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Tukianza na Siku ya Uhuru wa Habari Tanzania, Waziri Mkuu Majaliwa amewataka viongozi na watendaji wa serikali waondoe ukiritimba kwenye suala la upatikanaji wa habari ili kuwawezesha wanahabari kupata taarifa sahihi na kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Anasema viongozi na watendaji wa serikali na mashirika wanapaswa kuzingatia Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa ya Mwaka 2016 na kuondoa ukiritimba katika suala la upatikanaji wa habari ili wanahabari wawezeshwe kupata taarifa sahihi na wafanye kazi zao kwa ufanisi wa hali ya juu.

Japo sheria ya upatikanaji taarifa imefungua milango ya upatikanaji habari ni haki, ukiritimba kwenye kanuni za utumishi wa umma kuhusu utoaji habari uko pale pale. Wasemaji wa serikali ni zuga tu kama matarishi. Badala ya kuwa wasemaji rasmi wa taasisi zao, wengi ni watoa taarifa tu licha ya kwamba kikanuni wasemaji wakuu ni watendaji wakuu wa taasisi hizo na si wasemaji.

Ukiritimba huu upo kuanzia msemaji wa Ikulu. Kazi ya msemaji wa Ikulu ilikuwa kutoa tu 'press release' na si kusema. Pongezi nyingi ziende kwa msemaji wa sasa wa Ikulu, si tuu anatoa taarifa kwa umma bali anasema na vipindi anatengeneza. Kinachofanywa na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, Zuhura Yunus, kifanywe na wasemaji wote wa serikali, wasiishie kutoa 'press release'. Waitishe mikutano na waandishi wa habari, waseme na vipindi vya taasisi zao wafanye. ukiritimba wa utoaji habari uondolewe kwenye kanuni ili wasemaji wa serikali waisemee serikali na taasisi zake.

Kuhusu habari za uchunguzi, Waziri Mkuu amesema uandishi wa habari hizo unahitaji rasilimali fedha za kutosha ili kutoa mafunzo na kuifanya kazi yenyewe.

Aliwaomba wadau wote muhimu, zikiwamo taasisi, asasi za kiraia na mashirika mbalimbali ya ndani na nje ya nchi, washirikiane na vyombo vya habari katika kufanikisha utafiti na uandishi wa habari za uchunguzi na kuvisaidia vyombo vya habari kukua kitaaluma na kiuchumi.

Hili ni eneo muhimu ambalo vyombo vyetu vya habari vinashindwa kutokana na kukabiliwa na ukata mkubwa wa rasilimali fedha, hivyo hakuna uhuru wa habari bila uhuru wa kiuchumi wa vyombo vya habari.

Waziri Mkuu amewahimiza wanahabari wote wazingatie uzalendo, weledi na maadili ya taaluma ya uandishi kwa kutoa mchango chanya kwa jamii kwa kuwa wasipofanya hivyo, tasnia hiyo inaweza kuwa chanzo cha kufifisha maendeleo na hata kuhatarisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa. Hili ni jambo muhimu sana. Katika hilo, anasema vyombo vya habari vinayo nafasi kubwa ya kuitangaza nchi pamoja na kuijengea taswira chanya kimataifa.

Anasema vyombo vya habari vimekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha uwekezaji, kutangaza vivutio vya utalii na kuchangia katika maendeleo ya uchumi wa taifa. Kutokana na kazi hiyo, kwa niaba ya serikali na wananchi, alivyipongeza vyombo vya habari katika kuutumikia umma.

Katika kuweka msisitizo, Waziri Mkuu anasema vina mchango mkubwa wa kuhamasisha jamii kuwananchi katika shughuli na utekelezaji wa mipango ya Serikali pamoja na kampeni muhimu za kitaifa. Anasema waandishi wa habari wana nguvu ya kuongeza sauti kwa jamii kuhusu mmomonyoko wa maadili, athari za kimazingira, kufichua rushwa na uzembe na kuunga mkono masuluhisho yatakayochochea maendeleo endelevu na ustahimilivu katika maeneo muhimu.

Awali, Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye, alisema hali ya uhuru wa vyombo vya habari nchini imeimarika ikilinganishwa na ilivyokuwa awali.

Licha ya kwamba alisema habo havijafikia vinakotakiwa kwenda, haviko kama ilivyo kuwa jana. Alibainisha kuwa hatua ya sasa iliyopigwa na vyombo vya habari ni kutokana na juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan hasa katika utekelezaji wa 4R.

Mkutano huo ulihudhuriwa na wadau mbalimbali wakiwamo mabalozi wa Marekani, Uswisi, Mwakilishi wa Umoja wa Mataifa, Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni, Asasi za Kiraia, wawakilishi kutoka Muungano wa Klabu 28 za Waandishi wa Habari Tanzania (UTPC), Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) na wanavyuo.

Wiki Ijayo nitawaletea Mkutano wa Jukwaa la Wahariri Tanzania.

**Wasalaam**
**Pascal Mayalla**
**+255 754 270403**

# Wahalifu dawa za kulevya wapeana taarifa kwa kutumia sauti ya pikipiki

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

WADAU wa ulinzi na usalama Manispaa ya Singida, mkoani hapa, wamefichua mbinu ya wauzaji wa dawa za kulevya namna wanavyopeana taarifa na wanunuzi kwa kutumia sauti za pikipiki zenye milio mikubwa kuwa mzigo umewasili.

Wakizungumza na Jeshi la Polisi mkoani hapa jana, wadau hao walisema wauzaji wa dawa za kulevya wamekuwa wakitumia pikipiki hizo ambazo bomba la moshi limetobolewa makusudi, kupeana taarifa na wanunuzi kuwa, waende kwenye vituo vya kununulia wanavyovijua.

Hayo yaliibuliwa katika kikao kilichoitishwa na Kamanda wa Polisi Mkoa huo, Amon Kakwale, kwa ajili ya kujitambulisha ambacho kilishirikisha viongozi wa dini, wenyeviti wa serikali za mitaa, viongozi wa masoko, madiwani, viongozi wa vyama vya siasa na wafanyabishara.

"Ziko pikipiki zinapiga kelele sana mitaani, niliwauliza watu kwenye kijiwe cha kahawa kule stendi ya mabasi, wakasema hawa wanatoa taarifa kwa wateja wao kwamba, mzigo wa dawa za kulevya umeingia kwa hiyo wanunuzi waende vituo vya ununuzi,"alisema Kalebi Mnkenyi, Meneja wa Kampuni Binafsi ya Ulinzi ya Salu.

Mkenyi alisema kundi la watoto wa mitaani ambao wapo katika Manispaa hiyo, nalo ni hatari katika uhalifu, na kuiomba serikali kupitia halmashuri kuweka utaratibu wa kuwarejesha kwa wazazi wao au ndugu zao.

Kamanda Kakwale akizungumza na viongozi hao, alisema suala la kulinda raia na mali zao ni jukumu la kila mwananchi, hivyo kinachotakiwa ni ushirikiano kwa Jeshi la Polisi, kwa kutoa taarifa za matukio ya uharifu.

"Dhima ya Jeshi la Polisi ni kumhakikishia Mtanzania yeyote awe salama na mali zake, ambapo jukumu hilo limekasimiwa kwa jeshi hili kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977," alisema.

Kamanda Kakwale alisema kwa kutambua kuwa Jeshi la Polisi pekee haliwezi kufanya lenyewe, mwaka 2006 lilianzisha mfumo mpya wa ushirikishwaji wa jamii na kuwa na mkakati wa polisi kata, lengo likiwa ni kusogea karibu na wananchi.

"Wananchi wa Manispaa ya Singida na mkoa huu kwa ujumla, tunapaswa kuondoa dhana kwamba, kazi ya kulinda mali ni ya Jeshi la Polisi pekee, tuone ni kazi ya wote, kwani hata Katiba Ibara ya 26, 27 na 28 inazungumzia wajibu wa kila Mtanzania," alisisitiza.

Kamanda Kakwale aliongeza kuwa, makosa ya unyanyasaji ambayo ni pamoja na ubakaji na ulawiti katika Mkoa wa Singida, yanaongezeka kila siku, hivyo ni jukumu la kila mwananchi kukomesha matukio hayo kwa kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili hatua ziweze kuchukuliwa.

"Wanaofanya makosa haya hawaishi mbingu nyingine, wapo mbingu hii hii, na wengine tunaishi nao, tupeni ushirikiano ili tuweze kupambana na makosa haya, watendaji waweze kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria," alisema.

Aidha, wadau hao waliliomba Jeshi la Polisi kuimarisha doria mitaani ili kukomesha vitendo vya vijana wanaokunywa pombe asubuhi na wengine kucheza kamali, badala ya kwenda kwenye shughuli za uzalishaji.

Kadhalika walimhakikishia Kamanda Kakwale kwamba, watampa ushirikiano wa kutosha katika kukomesha uhakifu mkoani humo, huku viongozi wa dini wakisema, wataendelea kuliombea Jeshi la Polisi, liweze kutekeleza vyema majukumu yake ya kulinda raia na mali zao.

# PM aungana na wana Dar kampeni ufanyaji mazoezi

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameshiriki mazoezi ya pamoja ya kampeni ya kitaifa inayoratibiwa na Wizara ya Afya, ya kuhamasisha ufanyaji wa mazoezi kwa watanzania ili kujiepusha na magonjwa yasiyoambukiza.

Amesema hatua hiyo pia, ni kuunga mkono wito wa Rais Samia Suluhu Hassan, wa kufanya mazoezi ili kujikinga na magonjwa hayo na kulitaka Jeshi la Polisi kuimarisha ulinzi wa eneo hilo ili liendelee kuwa salama.

Majaliwa aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam aliposhiriki katika kampeni hiyo pamoja na matembezi ya kilomita 10 yaliyoanzia katika fukwe za Coco kupitia Daraja la Tanzanite hadi Ocean Road.

"Mnakumbuka programu hii iliyoanzishwa na Rais Samia Suluhu Hassan, na yeye mwenyewe kushiriki na kuwahamasisha watanzania kushiriki mazoezi mbalimbali, katika kipindi cha miaka mitatu ya Rais moja ya mambo ya kujivunia ni mafanikio katika sekta ya michezo," alisema. Majaliwa alitoa wito kwa viongozi wa Manispaa ya Kinondoni kufanya maboresho zaidi katika eneo la fukwe za Coco Beach ili liwe safi na livutie watu wa rika mbalimbali.

"Nawapongeza Jeshi la Polisi kwa kazi nzuri ulinzi katika eneo hili, nitoe wito kwenu kuendelea kuimarisha ulinzi ili eneo hili liwe salama kwa watu wa rika na jinsia zote, aliagiza.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alimshukuru Waziri Mkuu kwa kukubali kushiriki katika mazoezi hayo, huku akitoa taarifa ya ongezeko la magonjwa 10 yasiyo ya kuambukiza jambo lililofanya wizara hiyo kuleta ombi la kuanzisha utaratibu huo kila Jumamosi.

"Mwaka 2022 kati ya magonjwa 10 yanayowasumbua watanzania, moja lililojitokeza ni shinikizo la juu la damu bajeti ya mwaka 2022/2023 likaongezeka na kisukari katika magongwa 10 yanayowasumbua watanzania. Wajibu wa Wizara ya Afya ni kuwakinga Watanzania wasipate magonjwa," alisema. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema mkoa huo utajipanga kuhakikisha utaratibu huo wa mazoezi unakuwa endelevu kwa kushirikiana na kamati ya ulinzi na usalama pamoja na wadau mbalimbali wa michezo.

# Mabaraza ya ardhi kwenda mahakama

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imeandaa mapendekezo ya kuhamisha shughuli zinazofanywa na Mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya kutoka Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwenda mahakama.

Waziri wa Wizara hiyo, Jerry Silaa, aliyesema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Rorya (CCM), Jafari Chege.

Katika swali lake, Mbunge huyo alihoji lini serikali itahamisha mabaraza hayo kwenda kwenye mfumo wa mahakama.

Silaa akijibu swali hilo, alisema katika jitihada za kuboresha mfumo uliopo wa utatuzi wa migogoro ya ardhi nchini, serikali kupitia Wizara ya Katiba na Sheria imeandaa mapendekezo hayo.

Katika swali la nyongeza, Mbunge huyo alisema Wilaya ya Rorya haina baraza la ardhi hali inayosababisha wananchi kusafiri umbali wa kilomita 60 hadi 100 kwenda Tarime kufuata huduma hiyo.

"Umbali huu unasababisha wananchi kukata tamaa kushughulikia haki zao za kimsingi za kisheria za utatuzi wa migogoro ya ardhi, je, serikali haioni haja ya kuanzisha baraza la ardhi Rorya,"alisema.

Alisema pia, kumekuwapo na kukithiri kwa vitendo vya rushwa kwenye mabaraza hayo na kuhoji mpango mkakati wa serikali wa kukomesha vitendo hivyo vinavyowanyima haki wananchi.

Waziri Silaa akijibu swali hilo, alisema kwasasa nia ya serikali ni kuondosha mabaraza hayo na kuyapeleka mahakama kutokana na mifumo ya utoaji haki kuboreshwa.

"Nikiri kumekuwa na malalamiko mengi ya tuhuma za rushwa kwenye mabaraza haya, wizara itakapopata taarifa mahsusi za baraza ambalo limefanya maamuzi ya shauri kwa kushawishiwa na rushwa tutachukua hatua,"alisema.

Hata hivyo, alisema wakati mchakato huo unaendelea wa kuhamisha mabaraza kwenye mahakama, kuna wilaya 36 hazina mabaraza na watakapopatikana wenyeviti mabaraza hayo yataanzishwa.

# Pinda awageuzia kibao maofisa TRA

**Na Munir Shemweta,** MLELE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda, ameitaka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kujenga uhusiano mzuri na wafanyabiashara wa eneo la Majimoto katika Halmashauri ya Mpimbwe, wilaya ya Mlele mkoani Katavi.

Pinda alitoa kauli hiyo juzi wakati wa kikao cha pamoja kati ya maofisa wa TRA Makao Makuu na wafanyabiashara wa eneo la Majimoto, kilichofanyika katika Halmashauri ya Mpimbwe.

Kikao hicho cha siku moja, kilitokana na kuwapo malalamiko kutoka kwa wafanyabiashara kuwa wamekuwa wakinyanyaswa na maofisa wa TRA, jambo walilolieleza kuwa limekuwa likisababisha usumbufu katika biashara zao.

"Mimi kama Mbunge wa Jimbo la Kavuu, niko tayari kutoa ushirikiano na TRA lakini ushirikiano huo uende sambamba na mamlaka kujenga uhusiano mzuri na wafanyabiashara,"alisema.

Pinda alisema ni wajibu wake kuhakikisha maisha ya wafanyabiashara katika eneo hilo yanakuwa rafiki na kusisitiza kuwa eneo hilo linapoteza wateja wengi na sababu ya kuwapo na uhusiano mbovu na walipakodi.

Pia aliwataka maofisa wa TRA katika eneo hilo kutokuwa na dharau kwa wafanyabiashara na kuhoji: "Unapomdharau mlipakodi unategemea kitu gani?" Alisisitiza mamlaka hiyo kutoa huduma nzuri kwa kwa wateja.

Kwa mujibu wa Pinda, lazima maofisa wa TRA wawe rafiki na wafanyabiashara ili kuondoa vikwazo vinavyoweza kusababisha mkwamo kwa wafanyabiashara.

Alibainisha kuwa TRA pamoja na mambo mengine, lazima ijikite kutoa elimu kwa mlipakodi kama maofisa wake walivyofanya kwa kwenda kwa wafanyabiashara wa Majimoto huku akiwataka kuacha kabisa siasa katika shughuli za kibiashara.

"Nasema haya ili mje na mageuzi makubwa kwa lengo la kuboresha," alisisitiza.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mpimbwe, Shamim Daud, alisema zaidi ya asilimia 50 ya mzunguko wa fedha katika halmashauri yake inatoka eneo la Majimoto ndiyo maana halmashauri imeweka uwekezaji mkubwa katika eneo hilo ili kuhakikisha huduma za jamii zinaimarishwa na kupunguza changamoto kwa watu wanaoingia na kutoka.

"Kwa hiyo tunashukuru na tunatumaini kikao hiki watu watakapotoka watakuwa wamejifunza na TRA watakuwa wameelewa changamoto za maeneo hayo na kuwaletea mabadiliko makubwa". Amesema Mhe, Pinda.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Geophrey Pinda akisisitiza jambo wakati wa kikao cha maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wafanyabiashara wa eneo la Majimoto, Halmashauri ya Mpimbwe, wilaya ya Mlele mkoani Katavi juzi. Kulia ni Mkuu wa wilaya ya Mlele, Alhaji Majid Mwanga na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo, Shamim Daud. **PICHA: WANMM**

# CCM yaahidi kuwa mtetezi wa wananchi wote

**Na Is-haka Omar.** ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Mohamed Said Dimwa, amesema Chama hicho kitaendelea kuwa mtetezi na mwangalizi wa wananchi wote.

Dk. Dimwa alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na kada wa CCM ambaye ni Mkurugenzi mstaafu Idara ya Umwagiliaji Wizara ya Kilimo Zanzibar, Dk. Ramadhan Abeid Ramadhan, nyumbani kwake, Fuoni.

Alisema lengo la ziara yake hiyo ni kumtembelea ili kumjulia hali ikiwa ni sehemu ya mwendelezo wa ziara zake za kuwatembelea makada,wazee na wananchi kwa ujumla. Ziara hizo, alisema zinaendeleza utamaduni wa CCM wa kuweka daraja huru la uhusiano mwema baina ya chama na wananchi bila kujali tofauti za kidini, kisiasa na kikabila.

"Kila nikikutana na wazee na makada wakongwe waliotumia nguvu na muda wao kuitumikia nchi yetu kwa uadilifu ,nafurahi sana kwani napata ushauri, mbinu na nasaha nzuri za kunisaidia katika masuala ya utendaji na kuwatumikia kwa ufanisi zaidi wanachama wa CCM na wananchi kwa ujumla.

"Dhamira ya CCM ni kushinda katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2025 ili tuendelee kuongoza nchi kwa uadilifu na ufanisi mkubwa kwa kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora zinazoendana na mahitaji yao ya sasa kiuchumi, kijamii na kimaendeleo,",alisema.

Naye Dk. Ramadhan alimshukru Dk. Dimwa kwa kumjali na kumtembelea kwa dhamira ya kubadilishana mawazo juu ya masuala mbalimbali ya Kijamii.

Dk. Aseid alimpongeza kwa dhati Dk. Dimwa kwa utendaji wake unaoleta ufanisi na mabadiliko mkubwa ya kiutendaji ndani ya CCM na jumuiya zake.

MAISHA
MEI 5, 2024
Nipashe
Baba, Mama na Mwana
Jumapili



Fahamu haya kabla ya kuuza nyumba

Ukurasa 15




# JUNI TUNAKWENDA HIVI...

Ukurasa 13

# WATOTO


## MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA



| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 8 | 5 | 2 | 7 | 1 | 3 | 8 | 8 | 4 |
| 8 | 6 | 7 | 5 | 6 | 4 | 8 | 0 | 0 |
| 1 | 8 | 8 | 9 | 9 | 9 | 6 | 6 | 9 |
| 6 | 6 | 1 | 5 | 3 | 6 | 8 | 3 | 9 |
| 3 | 4 | 0 | 2 | 9 | 5 | 0 | 6 | 1 |
| 7 | 0 | 4 | 3 | 7 | 1 | 2 | 0 | 5 |
| 6 | 8 | 0 | 8 | 2 | 5 | 6 | 2 | 1 |
| 1 | 4 | 2 | 2 | 8 | 7 | 4 | 7 | 2 |
| 2 | 6 | 7 | 5 | 4 | 9 | 9 | 4 | 7 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| S | ■ | P | E | M | B | A |
| H | ■ | ■ | ■ | K | ■ | B |
| E | ■ | P | A | O | ■ | W |
| R | A | I | ■ | S | A | A |
| E | ■ | M | E | I | ■ | G |
| H | ■ | B | ■ | ■ | ■ | W |
| E | L | I | M | U | ■ | E |


## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyo wazi:

ILA, ZII, FAA, BAA, IGAWE, KUNDI, NDAZA, FAIDA, JAMBAZI, IMBISHA

## TOA TOFAUTI 5




## AMSHA AKILI

NGOJA LEO TUONE UWEZO WAKO WA KUMUDU SOMO LA KIINGEREZA DARASANI. TAFUTA MAJINA YAFUATAYO KATIKA JEDWARI HAPA CHINI:

DAD MOM BABY BOY GIRL FAMILY

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| X | M | B | I | D | A | D | K |
| V | S | O | Z | N | F | Q | M |
| G | D | Y | E | J | H | R | O |
| I | F | A | M | I | L | Y | M |
| R | B | P | L | C | W | U | G |
| L | A | T | O | B | A | B | Y |

## PAKA RANGI




## CHEKA



Alichokifanya daktari

TOFAUTI ya wazazi wa hapa nchini mtoto wa Tanzania na sehemu zingine wakati anapolala inakuwa kama hivi.

Marekani mtoto anapokwenda kulala huagwa na wazazi wake “usiku mwema mwanagu”

Uingereza wazazi wanamuaga mtoto wao “Pata njozi njema mwanetu”

Hispania anapokwenda kulala wazazi humuaambia “usiku mwema mpendwa wetu”

Tanzania mtoto anapotaka kulala wazazi utawasikia “Kesho umke mapema, hatutaki kusikia umechelewa na hela ya mihogo utaikuta mezani”

**SWALI**

Makaa yam awe yanapatikana wapi hapa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO
Na Flora Wingia



# Hiki ndicho chanzo cha matatizo ya ndoa nyingi

KARIBU tena msomaji wangu tuendeleze mada kuhusu mitikisiko katika ndoa nyingi hata kusababisha zingine kubomoka na kila mwanandoa kuanzisha maisha mengine.

Wiki iliyopita tulijadili kwa nini shetani anashambulia sana ndoa? Nilitaja maeneo mawili, moja likiwa ni ujinga kwa baadhi ya wanandoa kutokuwa na maarifa namna ya kuishi katika ndoa.

Nikataja kupuuzia kanuni na misingi ya ndoa. Ukitaka uwe na ndoa yenye mafanikio na upenyo ni lazima utendee kazi kanuni na maelekezo yote yanayohusu ndoa.

Kwa bahati mbaya sana, watu wengi walioko kwenye ndoa hupuuza na kutupilia mbali kanuni na maelekezo waliyopewa siku wanafunga ndoa. Unapopuuzia kuombea ndoa yako, unapoanza kuona mabadiliko kwa mumeo au mkeo unapuuzia, hiyo itakugharimu baadaye.

Unapoota ndoto mbaya kuhusu mumeo au mkeo na kupuuzia, unaweza kujikuta unaingia kwenye matatizo makubwa ya ndoa baadaye.

Leo msomaji wangu tuende zaidi kuangalia chanzo cha matatizo ya ndoa. Nitajitahidi kuchambua vyanzo mbalimbali kadiri itakavyowezekana ili kusaidia wanandoa wengi ambao wana maswali mengi kuhusu mitikisiko katika ndoa zao wasijue cha kufanya.

Ni vema ikaeleweka kwamba kila tatizo la ndoa lina chanzo. Moja ni zile ndoa zinazofanyika pasipo Mungu kuhusika. (wakati ulikuwa adui wa Mungu). Watu wengi ambao huanza maisha ya ndoa pasipo kumshirikisha Mungu hukumbana na matatizo makubwa ya ndoa.

Siku zote msingi mbaya wa nyumba husababisha jengo kuwa dhaifu. Uhusiano wowote uliofanya wakati ukiwa adui wa Mungu huwa unafeli.

Mwanaume yoyote aliyeokoka na kuchukua maamuzi ua kumuoa binti ambaye hajaokoka, hujisababishia matatizo yeye mwenyewe huko baadaye. Ipo hivyo pia kwa binti kuolewa na mtu asiyeamini upo uwezekano wa matatizo baadaye.

Ndiyo maana Mungu akasema katika moja ya maandiko yake kwamba, "Msifungiwe nira pamoja na wasioamini, kwa jinsi isivyo sawasawa; kwa maana pana urafiki gani kati ya haki na uasi?"

Chanzo kingine ni pale ndoa inapofungwa kwa sababu tu ya kupata mimba kwa bahati mbaya/kumpa binti mimba. Watu wengi leo wameoana siyo kwa sababu walipanga, bali kwa sababu walilazimishwa kutokana na kupeana mimba kwa bahati mbaya.

Ndoa za aina hiyo hazifanyiki kwa sababu ya upendo bali kwa sababu ya matokeo ya kile walichokifanya. Aina hii ya ndoa inaitwa "zimamoto". Kama umewahi kuona watu wa zimamoto wanavyofanya kazi kwa haraka sana na hawana muda wa majadiliano.

Binti anapopata mimba tu, kila mtu huanza kutaharuki. Wazazi wa pande zote mbili hukaa kwa haraka na kukubaliana ndoa ifungwe kwa haraka sana ili wasipate aibu.

Aina hii ya ndoa hutokana na tamaa ya mwili na siyo upendo wa dhati. Kama ungekuwa ni wa kweli binti asingejikuta ameingia katika matatizo ya namna hiyo.

Chanzo kingine ni kujihusisha kimapenzi kabla ya ndoa. Imebaika kwamba mapenzi kabla ya ndoa husababisha matatizo makubwa sana ya ndoa leo na kufanya mtu ajijengee majeneza ya kuzimu. Kama ukijenga jeneza kwa ajili ya ndoa yako, lazima utazikwa huko!

Vijana wengi leo wameshindwa kutunza ujana wao. Mabinti wengi nao wanaaibisha wazazi wao. Wengi wanaingia vyuoni, lakini wanapohitimu wanakuwa ni makahaba waliofuzu!

Chanzo kingine kinatokana na ndoa zilizofungwa baada ya mtu kwenda kwa mganga wa kienyeji. Ni kawaida katika tamaduni za baadhi ya wazazi wa Ki-Afrika kutembelea waganga wa kienyeji ili wawabashirie hatma za watoto wao.

Na mara zote, watu wengine wanaoamini huenda kwa wazazi wao na kuwaambia kwamba Bwana amewaongoza kuoa watu wa aina fulani. Ndipo wazazi huchukua majina ya wachumba wao na kuyakimbiza kwa waganga ili wajue kama ni mke/mume sahihi wa watoto wao.

Kama wewe ni mchunguzi msomaji wangu, wazazi wengi wa ki-Afrika, wana tabia ya kuchukua majina ya watu wanaowazunguka watoto wao. Kama ndoa yako ilifanyika katika misingi hiyo, haitafika mbali. Shetani ni mjanja sana. Anatumia historia ya maisha yako kupambana na maisha ya ndoa.

Leo tuishie hapa tuendelee wiki ijayo, nikutajie vyanzo vingine zaidi vinavyotesa ndoa nyingi katika jamii yetu. Bila shaka umejifunza kitu hapo.

**Je, una maoni au kisa cha kimaisha? Ujumbe mfupi 0715268581.**

## WARAKA WA NDANI
Na Godfrey Mushi



# Usijisifie ya kesho, hujui yatakayozaliwa ndani ya ndoa yako

LITRUJIA ya kufunga ndoa inayotumiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), inatoa nafasi ya kila anayetaka kufunga ndoa kuweka ahadi au kiapo.

Tulioko ndani ya ndoa tunakumbuka maneno haya, "Mimi Vicent, nakubali na naweka ahadi ya kuoana na wewe, Selina, kuwa mke/mume wangu kwa maisha yetu yote. Niwe nawe tangu leo hii (yaani niambatane nawe) katika mema na mabaya, katika hali ya utajiri na umaskini, katika ugonjwa na hali ya kuwa na afya; nikupende, nikutunze mpaka kifo kitakapotutenganisha kufuata agizo takatifu la Mungu.

"Hii, ndiyo ahadi yangu ya kweli mbele yako, na mbele ya Mungu na Usharika huu".

Ndoa ni agano, si mkataba. Ndoa ya kikristo ni agano ambalo watu wawili wanawekeana. Mkazo wa agano ni uaminifu wa yule anayeliweka, kulitunza na kulidumisha katika hali zote.

Kwenye agano, mkazo si nataka nifanyiwe hiki na kile. Kwanza ili nidumishe agano; bali mimi nifanye nini kwa mwenzi wangu, ili agano lidumu.

Neno agano lililotumika katika Biblia (Berith kwa Kiebrania) mkazo wake ni kuunganisha au kufungamanisha pamoja na tunapozungumzia ndoa ni kwa mwanamume na mwanamke.

Kumbuka hili, mwanadamu anaweka agano na mwenzi wake, kisha Mungu analiweka muhuri lile agano ya kuwa halitabadilika wala kubadilishwa tena. Ni la kudumu.

Mkataba ni makubaliano ya watu wawili au zaidi, wanaowekeana masharti na sheria za kufuata ili mkataba udumu. Mkazo wake ni ya kwamba mmoja akivunja masharti na sheria, mkataba unavunjika kisheria.

Atakayevunja ataadhibiwa kisheria na kuna uwezekano mkubwa asifaidi chochote. Mkataba husimamiwa kwa sheria, si upendo.

Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 ya Tanzania inatambua aina tatu za ndoa. Ndoa ya kimila, ndoa ya serikali na ndoa ya kidini. Kila aina ya ndoa ina taratibu zake. Mfano, kuna aina za ndoa zinazofungwa zinazoruhusu mwanamume kuwa na mke zaidi ya mmoja. Serikali inatambua hilo.

Ndoa ya Kikristo, pamoja na kuwa ni ya mke mmoja na mume mmoja, pia inasimamia maadili ya Kikristo kulingana na neno la Mungu. Sheria ya Ndoa ya Tanzania, haikazii juu ya agano. Agano ni jambo la kibiblia, jambo la kimungu.

Kwa sababu ni sheria, imeweka vipengele 10 ambavyo mwanandoa akivivunja, ndoa yake inaweza kuvunjwa kisheria na kutoa hati ya talaka.

Baada ya kupewa hati ya talaka, wana ndoa hawa wakija kanisani, wanakumbushwa upya ahadi ya ndoa waliyoiweka kwa maisha yetu yote.

Je, maisha yote ndio yameishia hapo? Je, kifo mlichoahidi kimetokea wapi? Bwana Yesu naye alisema alichokiunganisha Mungu, mwanadamu asikitenganishe.

Hapa niache uwanja wazi wa majadiliano kwa wanandoa. Je, cheti cha talaka cha Mahakama kinatosha kuwa sababu ya kuvunja ndoa ya Kikristo?

Hakuna ajuaye kesho ya mwenzi wako. Maandiko yanatuonya kwa kusema, usijisifu kwa ajili ya kesho kwa maana hujui yatakayozaliwa na siku moja. Mith 27:1

Mara nyingi wana ndoa wanaanza ndoa zao wakiwa na afya njema, na matarajio chanya ya siku za usoni. Wako wanawezeshwa na Mungu kuanza ndoa wakiwa na mali na fedha za kutosha kujikimu.

Kipindi hiki mwa mwanzo wa ndoa, huwa cha amani, furaha, upendo na ushirikiano. Maneno kama, nyumba yetu, shamba letu, watoto wetu, fedha zetu au mipango yetu, ni ya kawaida kabisa kwenye ndoa hii changa.

Hali ya ugonjwa, inawezekana akapata ugonjwa usioponyeka haraka au akapata ulemavu utakaomfanya awe tegemezi kwa mwenzi wake.

Hapa tuliweka agano la kuwa naye katika hali ya ugonjwa. Mungu aendelee kuwabariki na kuwatia nguvu wale ambao, wenzi wao walipopita au bado wanapita katika kipindi kama hiki, bado wanasimamia agano lao.

Wengine wamewatelekeza kwa ndugu na marafiki kwa kisingizio chochote kile.

Kuhusu hali ya umaskini, safari ya maisha ya ndoa, huweza kuanza kuonyesha kwamba, kuna mmoja anayechangia zaidi kipato cha nyumbani kuliko mwingine. Shetani akapanda kiburi ndani ya mwanandoa huyu na akaanza kumlaumu mwenzake kwamba yeye ni 'golikipa' tu.

Inawezekana kuongezeka kipato cha mmojawapo ni baraka, ambayo Mungu aliikusudia kwa wanandoa hao. Mfano, mmoja wao alipata nafasi za kujiendeleza kimasomo, na hiyo ikamwongezea kipato. Au mmojawapo akafanikiwa zaidi katika biashara walioianzisha pamoja. Au mmoja akapata mafao fulani.

Lakini pia kipato cha mwenzi mmoja kinaweza kushuka au kutokuwepo kabisa, kwa sababu yoyote ile, iwe ugonjwa, kufukuzwa kazi, kuibiwa au biashara kutokufanikiwa.

Kiburi na majivuno yanaweza kumwingia yule anayefanikiwa, akasahau agano la wakati wa umaskini. Wanandoa wengine, wanatumia nafasi hii kuwanyanyasa, kuwasema vibaya, na mara nyingine kuwakimbia kabisa na kuanza mfumo mpya wa maisha bila kumjali mwenzi wake.

Mara ngapi umesikia mume au mke akitamka ya kuwa huyu mwenzi wangu ni kisirani au nuksi au mkosi? Au umewahi kusikia mara ngapi, wakwe wakisema huyu mke wa kijana wetu ni mkosi. Tangu ameolewa na mtoto wetu, hana maendeleo yoyote.

Kwanza, mwanandoa nikutoe hofu. Kama unamwamini na kumtegemea Mungu, baraka za bwana zitakuandama wewe na nyumba yako, mjini na mashambani. Lakini katika safari ya ndoa, mabaya yanaweza kuwapata. Sikiliza maneno mabaya yalipoandamana na Ayub, na hata mkewe kumdhihaki.

Alisema wewe wanena kama mmoja wa nawawake wapumbavu wanenavyo. Je, tupate mema tu mkononi kwa Mungu, asi tusipate na mabaya? Soma Ayubu 2:10.

Mabaya yanapotujia katika ndoa, tusilaumiane. Turudi kwa Bwana na kumsihi atuondolee mabaya. Kama mabaya yalikuja kwa sababu ya dhambi zetu, toba ni lazima.

Fundisho hili limkumbushe kila mwanandoa kusimama katika agano lake la ndoa kwa gharama yoyote.

• **Godfrey Mushi, ni Mwandishi Mwandamizi wa Nipashe, Kanda ya Kaskazini. Anapatikana kwa barua pepe: ghandsome79@gmail.com. Simu ya mkononi: +255 715 545 490**

# HARUSI



Kumbukumbu iliyotukuka kwa wanandoa Godson Mafita na mkewe Theopista Mzena walipofunga ndoa katika kanisa la Calvary Asemblies of God, jijini Dodoma na sherehe ilifanyikia ukumbi wa kanisa hilo.









# MITINDO

Na Moshi Lusonzo

## JUNI TUNAKWENDA HIVI...

KATIKA kukabiliana na hali ya baridi linalotokana na kipindi cha kipupwe kinachotarajiwa kuanza hivi karibuni, mavazi yanayoongeza joto yanahitajika kila wakati.

Kulingana na hali ya baridi la wastani, vazi la jaketi lina umuhimu wake hasa katika kuweka mwili katika hali joto iliyo sawa na hatimaye kuendelea kufanya shughuli zako bila usumbufu.

Kimsingi ndani ya nyumba ni muhimu kuwa na jaketi hata moja kwa sababu licha kuwa kama kifaa cha kukuongezea joto, ni vazi lenye mwonekano mzuri.

Wabunifu wamefanya marekebisho mengi kwa ajili ya kuendana na kasi ya teknolojia na mwenendo wa vijana

Sifa kubwa ya nguo hizi ni kuwa na uwezo wa kutengeneza joto wakati wa baridi na pia lina mwonekano wa kuvutia pale mtu anapovaa.

Majaketi yana kawaida ya kutochagua aina zingine za nguo za kuvaa, Mfano unaweza kuvaa na suruali ya jeans, suruali ya kitambaa au nguo ya mazoezi.

Usisahau ukitaka kupendeza zaidi pigilia viatu vyako vya kutumbukiza kama raba, buti na viatu vingine unavyopenda.





URAMBO

## UREMBO

Na Mary Geofrey

UNA MIAKA 50?

# Zingatia haya kutunza mwili



KILA mwanamke mwenye zaidi ya miaka 50, anakumbana na matatizo mbalimbali ambayo yanapunguza mwonekano wa uzuri wake.

Katika umri huo kuna mambo mengi unatakiwa kuyafanya ili kuboresha afya ya mwili wako. Hizi ni baadhi ya hatua dalili unazotakiwa kujua kuwa mwili wako unahitaji kuboreshwa.

**Tayarisha ngozi kavu**

Ukavu wa ngozi ni ishara kwamba kuna tatizo la ukosefu wa virutubisho fulani vinavyofanya ngozi kuwa laini.

Kwa hiyo ni muhimu kutumia kifaa cha unyevushaji na usitumie sabuni na mafuta ya ngozi

Unapaswa pia kushauriana na daktari ikiwa una matatizo yoyote.

**Kula, kunywa maji mengi**

Kula chakula cha afya pia huboresha afya ya ngozi. Kunywa maji mengi kwani husaidia kulainisha ngozi kutoka ndani kwenda nje.

**Tumia mafuta**

Ikiwa una zaidi ya miaka 50, marashi na dawa zingine za ndani zinaweza kusaidia kuboresha afya ya mwili wako.

Mafuta ya kulainisha ngozi, yatasaidia seli za ngozi yako kuzalisha kolajeni ambayo inakuza uzuri na ubora wa ngozi.

**Mazoezi**

Mazoezi husaidia kuongeza afya na uchangamfu wako, pia kuzuia unene ambao ni moja ya sababu za kuzeeka mapema, pamoja na matatizo ya kiafya ambayo unene husababisha.

Usile sana kabla ya kwenda kulala, kwa sababu hii inaweza kusababisha kula sana na kutokuwa na uwezo wa kuvaa mavazi mengine hadharani.

**Nywele**

Nywele ni sehemu muhimu ya uzuri na kujistahi kwa mwanamke, hasa akiwa na umri wa zaidi ya miaka 50, wakati nguvu, uzuri na kimo chake hupungua.

Kwa hiyo, unahitaji kutunza nywele zako vyema wakati huo huo nywele zikianza kubadilika rangi na kuwa kijivu.

## MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Juisi ya nanasi na maji ya nazi



BAADHI ya watu hupata ugumu kunywa maji ya nazi, lakini yanaweza kutumika kama kinywaji kitamu cha juisi na ukapata faida nyingi kiafya.

Juisi ya nanasi na maji ya nazi ina faida nyingi ikiwamo kuongeza nguvu kwa wanaofanya mazoezi na kuchochea mmeng'enyo wa chakula.

Pia, juisi hii inasaidia kuchochea mlinganyo wa hisia (mood) huku kwa wanaopenda ngozi zao, ikiwapatia mng'aro wa aina yake.

Una sababu gani ya kutonunua nanasi lako la buku na nazi ya 500 walau mara mbili kwa wiki na kupata faida hizi.

**Jinsi ya kutengeneza**

Chukua nanasi zima, anza kulimenya vipande vidogo vidogo na kisha weka kwenye blenda ya kusagia.

Anza kusaga hadi liwe laini sana na toa uanze kuchuja juisi yako, ukimaliza chukua maji ya bazi ambayo ushachuja vizuri na anza kuchanganya na juisi yako.

Kama nanasi litakuwa na ugwadu utaongeza sukari kidogo na uanze kuenjoy kinywaji hiki.

MAISHA NI NYUMBA

Na Elizabeth Zaya

# Fahamu haya kabla ya kuuza nyumba



BIASHARA ya nyumba na uwekezaji wa majengo ya kisasa inaendelea kushika kasi kila siku.

Mshauri wa uwekezaji masuala ya majengo, Abedi Charles, anasema kabla ya kuuza nyumba ni bora ufanye tathmini ya lengo na sababu ya kufanya hivyo ili uamuzi uwe sahihi.

Miongoni mwa mambo ya kuzingatia kabla ya kufikia uamuzi wa kuuza nyumba ni lazima utathmini lengo au sababu kuu ya kufanya hivyo.

Anasema wakati wa sasa, biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo unafanyika kwa mbinu za kisasa ambazo ni matokeo chanya ya ukuaji wa sekta hiyo ya ujenzi inayotokana na mapinduzi ya teknolojia mbalimbali duniani kote.



"Watu binafsi, kampuni na taasisi nyingi zimejitokeza kwa wingi kuzitumia fursa zinazoendelea kujitokeza kila siku kwenye biashara ya nyumba na uwekezaji wa majengo hususani kwa kuiendesha kisasa zaidi kwa kutoa huduma za makazi na biashara kwa wadau mbalimbali," anasema Charles.

Anaongeza kuwa: "Lakini kuna baadhi ya watu wamejikuta wakiingia kwenye uuzaji wa majengo yao kutokana na changamoto mbalimbali wanazokabiliana nazo kwenye maisha, na ndiyo maana ninashauri kwamba ni muhimu sana ukajitathmini kabla ya kuuza nyumba yako, je ni kwa lengo la kibiashara au kutokana na kushindwa kukabiliana na msukosuko wa changamoto za maisha zinazokukabili.

"Kutulia na kujitathmini kutakusaidia ufikiri vizuri na wakati mwingine kuepuka majuto kama hukuwa na ulazima wa kuuza nyumba yako."

Jambo linguine, anasema kabla ya kufanya uamuzi huo wa kuuza nyumba ni vema kutathmini bei na gharama ya mauzo ambayo unayapeleka sokoni ili kukusaidia kufahamu kiwango halisi na faida au mapato utakayopata kwa kutimiza malengo unayokusudia.

Mtaalam huyo anashauri kwamba ni muhimu kuzingatia kwa kuhakikisha nyumba yako inakuwa na muonekano mzuri na kushawishi wanunuzi na kwamba kama rangi yake ilikuwa imechakaa ni vema kuipaka upya pamoja na kuzingatia kuwa inakuwa safi wakati wote.

Anasema mvuto wa nyumba nao utakusaidia kukuongoza pia katika namna ya kufanya tathmini ya bei na itasaidia inunuliwe kwa muda mfupi.

Pia anashauri kwamba kabla ya kufanya uamuzi wa mauzo, ni vema kutathmini hali ya soko la nyumba na si kukurupuka.

Na Restuta James

# Pamba kwa meza ya bufee



SEHEMU ya kulia chakula ni moja ya eneo muhimu ndani ya nyumba yoyote na ndio maana mtu anapojenga nyumba anazingatia eneo hili.

Mtaalamu wa mapambo ya ndani, Simon Alex, anaeleza kuwa mabadiliko makubwa yanayoendelea kwenye sekta nyingine yameigusa pia sekta ya nyumba na mazingira kwa ujumla, akizungumzia eneo la chakula.

Akizungumzia meza ya bufee, anasema chakula hakipaswi kuwekwa kwenye meza ya chakula watu wanapokaa na kula.


Badala yake, anasema meza ya bufee ndio inayopaswa kuwekwa chakula na inatakiwa iwekwe pembezoni mwa meza ya chakula ili iwe rahisi kwa mtu anapopakua chakula kufika mezani kula.

Anasema meza hiyo inapaswa kuwa ndefu kiasi na sharti iwe na kioo kikubwa ili mtu anayepakua chakula aweze 'kutupia' jicho kujitazama.

Meza hii inaweza kuwekwa mshumaa, ua na glasi nzuri za maji, juisi na matunda, ili mtu anayesubiria chakula aweze kujipooza na kinywaji au tunda alipendalo.

Kwa mujibu wa Simon, mbali ya kuweka chakula, meza ya bufee ni 'pambo' nzuri ndani ya nyumba kwani inaongeza unadhifu na 'kupunguza' vyombo kwenye meza ya kulia chakula.

## KATUNI


KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2024
SMS - 0713 447766
JUKWAANI
'CHEO'
"HEEEE?!
MTEJA ,MUADILIFU KAMA MIMI NINAYETUMIA MPAKA LAKI TATU PAPO KWA PAPO SIKU NIKIWA SINA KITU?
ATUKOPESHI
KAUNTA
TULIKUCHAGUA UKIWA MWEMBAMBAAAAAAA! NASHANGAA KERO KIBAO UNANENEPEANA!
THATHA KERO THI'DHAKWENU MIE NAKONDAJE?
AKKA! MWANAKWETU ETI' OOH! ANAUBAKA USUKANI...HAMNA HATA HAYA? MSINISIMANGE
DALADALA
SHEREHEKEENI SIKUKUU NA MKIPATACHO NA SIO MKITAKACHO... MABUCHA YAONENI KAMA MAPAMBO
'HOVYO!'
MWENYE MKEWE HAJASAFIRI KWENDA POPOTE NA ROHO BADO INAMUUMA
ILIPATA KIDONDA AU MICHUBUKO?
*KINYUNYIZO CHA LEO...
...SAFU HII INAWATAKIA PASAKA NJEMA MASHABIKI WAKE WOTE...

HABARI KIMATAIFA

# Rwanda, M23 walaumiwa mauaji ya wakimbizi Goma

**WASHINGTON,** MAREKANI

Marekani imeilaumu nchi ya Rwanda na kundi la waasi la M23 kwa kushambulia kambi maalum ya watu waliokimbia makazi yao na kusababisha vifo vya watu tisa.

Katika tukio hilo lililotokea katika kambi ya Mugunga mashariki mwa mji wa Goka nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), miili ya watu ilionekana imelela chini kwenye kambi hiyo wakiwemo watoto saba.

Hata hivyo, Jeshi la Congo na waasi M23 wanalaumiana kuhusu shambulio hilo.

Nchi ya Rwanda ambayo inapakana na DR Congo, inashutumiwa kwa kuunga mkono kundi la waasi, jambo ambalo inakanusha.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani, ilieleza kwamba shambulizi hilo lililotokea Ijumaa lilitoka katika maeneo yanayoshikiliwa na Jeshi la Rwanda (RDF) na kundi la M23.

Msemaji wa wizara hiyo, alisema nchi yake ina wasiwasi kuhusu utekaji wa maeneo zaidi uliofanywa na vikosi vya Rwanda na waasi wa M23 mashariki mwa DRC na kuzitaka pande zote mbili kuheshimu haki za binadamu na sheria za kimataifa za kibinadamu.

"Ni muhimu kwamba mataifa yote yaheshimu mamlaka ya kila mmoja na uadilifu wa eneo na kuwawajibisha wahusika wote kwa ukiukaji wa haki za binadamu katika mzozo wa mashariki mwa DRC," ilisema taarifa hiyo. Picha zilizosambaa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha miili ikiwa imelala chini kwenye kambi hiyo baada ya shambulizi la makombora.

Wakazi wengi walikimbilia katika kambi hiyo kuokoa maisha yao kutokana na mapigano yanayoendelea katika miji na vijiji vyao.

Msemaji wa jeshi la DRC, Lt. Kanali Guillaume Njike Kaiko, alisema shambulio hilo limefanyika kama kulipiza kisasi baada ya mashambulizi yaliyofanywa na vikosi vya serikali dhidi ya maeneo yanayokaliwa na jeshi la Rwanda.

Rais Felix Tshisekedi, ambaye alikuwa katika ziara kwenye mataifa ya nje, atarajea leo.

Hivi karibuni, waasi na wanajeshi wa serikali wameshutumiwa kwa vitendo vya unyanyasaji dhidi ya raia wakati wanapigania udhibiti wa maeneo.

Shambulio la hivi karibuni limetokea siku chache baada ya wapiganaji wa M23 kudai kuwa wameuteka mji wa Rubaya, eneo ambalo ni kitovu cha uchimbaji madini ya Coltan yanayotumika kutengenezea simu za mkononi na betri za magari yanayotumia umeme.

Wakati huo huo, mahakama ya kijeshi mjini Goma imewahukumu kifo wanajeshi wanane wa DRC kwa makosa ya utoro na uoga wakati wa kupambana na vikosi vya waasi wa M23 ambao wanatoka kabila la Watusi.

Wataalamu wa Umoja wa Mataifa walisema kuwa kundi hilo linaungwa mkono na nchi jirani ya Rwanda, ambayo pia inaongozwa na Watusi.



Waandamanaji wanaopinga vita Ukanda wa Gaza wakiwa kwenye kampasi ya Chuo Kikuu cha George katika jimbo la Washington nchini Marekani jana. **PICHA: AP**

## Uingereza yapanga muda kuwasafirisha wahamiaji

**LONDON,** UINGEREZA

SERIKALI ya Uingereza imeiambia Mahakama Kuu ya nchi hiyo kwamba safari za kwanza za ndege za kuwahamishia waomba hifadhi kwenda nchini Rwanda zitaanza Julai.

Jaji wa mahakama hiyo, Martin Chamberlain, alifichua kuwa Julai mosi hadi 15 safari hizo zitaanza.

Kauli hiyo aliitoa wakati alipokuwa akipanga siku ya kusikilizwa kwa pingamizi dhidi ya uhamiaji.

Pingamizi hilo liliwasilishwa na chama cha wafanyakazi wa umma nchini humo. Sheria mpya ya uhamiaji inaruhusu mawaziri kupuuza sehemu za sheria za ndani na za kimataifa wakati wa kuamua juu ya uhamishaji huo wa lazima kwa waomba hifadhi.

# Makubaliano kusitisha vita vya Gaza yanukia

**CAIRO,** MISRI

HUENDA makubaliano ya kusitisha mapigano kati ya kundi la Hamas na Israel, yatafikiwa hivi karibuni na kutoa nafasi kuachiliwa kwa wafungwa wa Kipalestina na mateka wanaoshikiliwa.

Ujumbe wa Hamas uliwasili mji mkuu wa Misri wa Cairo jana kwa ajili ya kuendelea na majadiliano ili kufikia makubaliano kuhusu mapatano ya amani na Israel katika Ukanda wa Gaza.

Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alisema hivi karibuni kuwa kikwazo pekee katika mapatano hayo ni kundi la Hamas ambalo linatakiwa kukubali.

Katika taarifa, Hamas ilisema iko katika nafasi nzuri ya kutafakari.

"Kwa kuzingatia mawasiliano ya hivi karibuni na wapatanishi nchini Misri na Qatar, ujumbe wa Hamas utasafiri kwenda Cairo Jumamosi kukamilisha majadiliano," ilisema taarifa ya kundi hilo.

Kundi hilo ambalo linatawala eneo la Ukanda wa Gaza tangu 2007, limedhamiria kukomesha uvamizi wa Israel.

Ofisa mkuu wa Hamas amethibitisha kuwa ujumbe huo uliwasili Cairo asubuhi ya jana utaongozwa na Khalil al-Hayya, ambaye ni kiongozi namba mbili wa tawi la kisiasa la kundi hilo katika Ukanda wa Gaza. Na kwa mujibu wa tovuti ya Axios, mkuu wa CIA, William Burns, aliwasili Ijumaa jioni, na kutoa ishara kwamba wakati wa maamuzi muhimu umefika baada ya miezi kadhaa ya mazungumzo.

Nchi wapatanishi ambazo ni Misri, Qatar na Marekani zimekuwa zikisubiri kwa karibu wiki moja jibu la Hamas kwa sharti jipya la kusitisha mapigano iliyowasilishwa mwishoni mwa mwezi wa Aprili.

Hata hivyo, wajumbe wa Hamas walitangaza kuondoka katika eneo la mazungumzo ya mwisho, kwenda Qatar ili kuliangalia kwa makini mkataba huo wa usitishwaji vita.

Katika mkataba huo, imewekwa vipengele vya kusitishwa kwa mashambulizi ya Israel na kuachiliwa kwa wafungwa wa Kipalestina ili kubadilishana na kuachiliwa kwa mateka waliotekwa nyara wakati wa shambulio la Hamas la Oktoba 7 kusini mwa Israel.

Hata hivyo, Hamas inasisitiza kuhusu usitishaji wa vita wa kudumu ambao Israel inakataa na kusisitiza kufanya mashambulizi ya ardhini katika mji wa Rafah hivi karibuni.

RFI

MAKALA

# MAMBO MUHIMU KATIKA KUANZISHA BIASHARA



Na Magabilo Masambu

**Jambo la tatu, usianzishe biashara ambayo hujawahi kuifanya kwa pesa za mkopo. Siku hizi umekuja mtindo wa vikoba, kupeana pesa kila baada ya muda fulani au unaamua kwenda benki kukopa fedha kwaajili ya biashara ambayo ni ngeni kwako, hakika utajuta hapo baadaye usifanye hivyo.**

LEO katika safu yetu, tuzungumze kuhusu biashara kidogo. Hii ni kwa sababu biashara ni Maisha. Kwa maana nyingine, maisha hayajakamilika bila kuuza na kununua. Lakini zaidi, wataalamu wa fedha wanasema kama huuzi chochote basi katika hatua za kuelekea kwenye mafanikio, utakuwa unazisikia tu kwa majirani.

Kwanza, tutakubaliana kwamba biashara yoyote huwa inaanza na wazo, lakini wazo bora lazima liwe limekusudia kutatua changamoto za jamii.

Mfano, umepata wazo la kuuza maji, maana yake unatakiwa kujua kama hilo ni tatizo katika eneo hilo.

Kwa hiyo jambo la kwanza kabisa, unapotaka kuanzisha biashara, unatakiwa kufanya utafiti au uchunguzi mdogo kuhusiana na wazo lako la biashara.

Utafiti huo utakuwa juu ya kutaka kufahamu changamoto kubwa waliyo nayo wananchi wa eneo hilo.

Biashara yoyote ambayo haitatui changamoto ya wakazi husika hata kama ungeifanya kwa miaka 100, hakuna siku utafanikiwa. Hii ni kwa sababu kama jambo ulilolanzisha si hitaji la watu, maana yake hutapata wateja wa kununua bidhaa zako. Badala yake watafuata bidhaa ambazo ni hitaji lao.

Utafiti utakuwezesha kufahamu wateja wako watakuwa kina nani. Usianzishe biashara kwa kutegemea yeyote atakayepita atanunua, ndiyo yeyote atakayepita anaweza kununua lakini wale wateja wako uliowakusudia waendelee kuwepo.

Jambo la pili, epuka sana kuanzisha biashara inayofanywa na wengi katika eneo hilo. Unaweza kuwa unaishi mahali fulani, jirani yako anauza vitumbua na wewe ni mmoja wa wateja wake.

Lakini kila siku unaona wateja ni wengi sana, wazo linalokuja kichwani mwako ni kwamba na mimi nikianzisha hapa, nitawapata kama yeye. Kitakachotokea kama utaanzisha maana yake mtagawana wateja. Kama alikuwa anapata Sh. 10,000 kwa siku, mtagawana na mwisho wa siku wote mtashindwa kuendelea na biashara.

Jambo la tatu, usianzishe biashara ambayo hujawahi kuifanya kwa pesa za mkopo. Siku hizi umekuja mtindo wa vikoba, kupeana pesa kila baada ya muda fulani au unaamua kwenda benki kukopa fedha kwaajili ya biashara ambayo ni ngeni kwako, hakika utajuta hapo baadaye usifanye hivyo.

Anza na mtaji mdogo ulio nao. Kwanza, utaanza kujifunza namna unavyopata faida hata kama ni kidogo lakini ukiweza kutunza hiyo faida ndogo na ukaweza kuikuza, basi katika biashara kubwa pia utafanya hivyo. Unapoanzisha biashara usiyo na uzoefu nayo, wakati huku kwenye kikundi au benki wanasubiri marejesho, kuna hatari ya kushindwa biashara hiyo na kuna wakati unaweza kugombana na wateja, ukidhani tatizo ni wao. Hatukatai kukopa ni jambo jema, lakini kopa wakati biashara tayari unaifahamu unajua faida yaze na wateja wako.

Jambo la nne, utamaduni na hali ya eneo. Bidhaa utakazouza lazima uzingatie utamaduni na hali ya eneo husika.

Usifunguwe biashara tu kwa sababu unataka kuonekana kwamba na wewe ni mchakalikaji na kwamba wenzako wakienda kazini na wewe unakwenda kwenye biashara, unaona aibu kubaki nyumbani bora ukae kwenye duka hata kama hakuna wateja.

Huwezi kufanya biashara ya nguruwe maeneo ambayo yametawaliwa na jamii ya Waislam au ukafanya biashara ya kanzu maeneo ambayo yametawaliwa zaidi na Wakristo au unafanya biashara za makoti ya baridi Dar es Salaam.

Jambo la tano ni kuhusu uhakika wa bidhaa zenyewe. Kwanza, uhakika katika ubora, pili uhakika wa namna rahisi ya kuzipata kwa mwendelezo.

Kwenye ubora wa bidhaa utakufanya uwe na wateja wa kudumu, wakishakuwa ni wa kudumu, maana yake hizo bidhaa zinatakiwa pia ziwe zinapatikana wakati wote.

Hakuna jambo baya kwa mteja kumwambia bidhaa zimeisha njoo siku fulani ujuwe huyo ushamkosa.

Jambo la sita, kabla ya kuanzisha biashara uwe na uhakika wa lugha utakayokuwa unaitumia kwa wateja wako, bila kujali kwamba ni wachache au watakuwa wengi kiasi gani.

Watanzania wengi tulivyo, huwa biashara ikiwa mpya na tupo katika harakati za kutafuta wateja huwa tuna tumia lugha nzuri sana, lakini tukishaona wateja wamezidi tunaanza lugha za dharau.

Mwisho kwa leo, ni juu ya matumizi ya fedha za biashara. Biashara nyingi zina faida kidogo, hivyo zinahitaji nidhamu ya hali ya juu, juu ya matumizi ya fedha. Ukiwa unafanya biashara huwezi kujua kwamba utafilisika ni mpaka utakapofirisika, kwasababu mtaji na faida inatabia ya kujichanganya pamoja. Huwa si rahisi kujua matumizi unayofanya tayari unatumia mtaji ni mpaka uishiwe.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**DAR ES SALAAM-TANZANIA.**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# *Narudi kwetu babu we, sikuzaliwa juu ya miti*



Na Adam Fungamwango

SIKU zote mwanamke akichoka huwa kiumbe tofauti na inavyofikiriwa. Mwanamke akimchoka mwanaume, utaomba ardhi ipasuke uingie.

Hata kama uliishi naye miaka 10, ile siku akisema kuanzia sasa hataki kuishi na wewe anaondoka ujue anamaanisha. Na akichoka ujue ni kweli maji yamemfika shingoni, amevumilia kila aina ya mateso na tabu, lakini ameshindwa kuendelea kumvumilia mwanaume.

Inaaminika kuwa wanawake ni viumbe wapole, na wavumilivu, wenye upendo, Mwanamke ndiye kiumbe pekee anayeweza kuishi na mwanaume mwenye mapungufu mengi kama ulevi, kupiga, gubu, uchoyo na vingine vingi vinavyofanana na hivyo, ambavyo kwa hali ya kawaida mwanaume asingeweza.

Kutokana na hali hiyo, baadhi ya wanaume huwachukulia poa. Na hata akimkosea, huomba msamaha na mwanamke akakubali. Wanawake ni wepesi pia kukubali msamaha wa mwanaume kuliko wenzao.

Kitu ambacho wanaume hawajagundua ni kwamba huwa wanahesabu. Mwanamke anaweka kumbukumbu kwa kila anachofanyiwa na kukiweka moyoni.

Kinachotakiwa hapo sasa usimvuruge, ukiendelea kufanya makosa ya mara kwa mara ya kujirudia, ipo siku isiyo na jina utapata unachokihitaji. Hutoamini macho na masikio yako kuona yule yule mkeo ambaye alikuwa anakutii, anabeba mapungufu yako yote, anakubali misamaha ya makosa mbalimbali mfululizo uliyomfanyia, amebadilika na sasa anachotaka ni kitu kimoja tu, muachane, umpe talaka yake aondoke. Na akishafikia hapo siku zote huwa hawarudi nyuma.

Ndiyo maana ukisoma Biblia, Waraka kwa Kwanza wa Petro 3:7, inasema hivi:

"Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili, na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu, na kama warithi pamoja wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe."

Hii ina maana kubwa na moja ambayo nitaisema hapa ni kwamba wanaume hawatakiwi kuishi na wake zao kimazoea. Mke ni lazima apendwe, ajaliwe, atunzwe na kulindwa.

Chochote mbali na hicho ipo siku unakuja kulia na kuomba siku zirudishwe nyuma ili umpe upendo uliokuwa haumpatii, pale atakapokuwa anakusaka kilicho chake na kuondoka.

Tena wanawake wa siku hizi siyo kama wale wa zamani, ambao hawaondoki mpaka umpe talaka, au mrudishwe kwa wazazi wake.

Wa kizazi cha sasa ananyanyua virago vyake, huyooo, kwa wazazi wake, anakwambia kabisa talaka itanifuata nyuma.

Ndugu yangu, hata kama huyo mke akirejea kwako, utakuwa umepoteza muda mwingi na gharama kubwa. Kikubwa hapa nawasihi wanaume vyema na wake zao au hata wapenzi wao.

Marijani Rajab aliyaona haya yametamalaki kwenye jamii na kutunga wimbo aliouita, 'Ndoa ya Mateso.'

Ni wimbo ambao unamzungumzia mama mmoja aliyechoshwa na manyanyaso na mumewe na akenda kwa mjumbe kuomba ushauri, ikiwemo kupewa talaka yake.

Tukio hili ni la kweli kabisa, ambalo Marijani alilishuhudia na maneno yaliyozungumzwa hapo yote yalitakwa na mama huyo mbele ya mjumbe. Mjumbe mwenyewe alikuwa mama yake Marijani.

Marijali alikuwa akisafisha redio yake uani kwao maeneo ya Kariakoo, Dar es Salaam, mara akaja mwanamke kwa mjumbe na kumwelezea yote. Kwa sababu Marijani alikuwa mwanamuziki, alivutiwa na maelezo ya mama yule, akawachukua na kuyatungia wimbo pamoja na maneno ya mjumbe ambaye ni mama yake mzazi.

kabla ya kurekodiwa, alikuwa akitaja mpaka jina la yule mama aliyemshtaki mumewe, lakini mama Marijani akamwambia mwanawe aondoe jina, na kumwambia akifanya hivyo watu wenye shida watakuwa wanaogopa kuja nyumbani kushtaki kwa kuogopa kutajwa redioni. Marijani akafanya hivyo, na hata uliporekodiwa haikuwa na jina la mama huyo. Mashairi ya wimbo huo ni huu hapa;-

"Niulizieni enyi walimwengu, huyu mwanaumume anavyonitesa, hii ndiyo haki au ni mateso, hii ndiyo haki au ni mateso? Kanitoa kwetu kwa baba na mama, kwa vigelegele na heshima nyingi, tizameni sasa anavyonigeuka, tizameni sasa anavyonigeuka.

"Ananipa mateso huku ugenini, sina hata ndugu wa kunisaidia, na mimi n'na watoto jamani tabu gani, na mimi n'na watoto jamani tabu gani. Kwani kuolewa ni jambo la ajabu? Au kuolewa sana ni utumwa? Kama ndiyo hivyo mimi nimeshindwa, kama ndiyo hivyo mimi nimeshindwa.

"Natoa ushahidi kwako we mjumbe, mwambie huyo bwana anipe talaka yangu, nisije kuondoka ikawa mateso, nisije kuondoka ikawa maneno.

"Mambo anayoyafanya ni aibu kusema, kwa kuwa leo nina uchungu nitakueleza. Hapa unavyotuona, hatuna chochote nyumbani, mume wangu haonekani sijui yupo wapi!

Anababaishwa na anasa za mjini, mimi kanitupa na watoto hawajali. Pesa zake zote zinaishia nje, kwa makuku ya kukaanga bibi na mkate mkavu. Nimechoka mimi na mwanamume mlevi, heri anipe talaka ili nirudi kwetu.

Sikuzaliwa juu ya miti, nikako kwetu, ninako kwetu kwa baba na mama.

"Mateso, mateso, mateso, yamezidi nachoka.

"Pole mama kwa tabu ulizozipata, lakini kwanza, usichukue hatua hiyo mama. Mimi na wazazi wake, tutamwita tumkanye, akirudia, mimi nitakuwa shahidi yako mama. Naona vibaya, mmeshazaa watoto, mkitengana, mtawapa tabu watoto wenu mama."

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

KIJANA Heri alikutana na msichana Nuru katika duka fulani maeneo ya Chanika, Dar es Salaam. Baada ya kuongea waliyoongea wakakubaliana kuonana siku ya Jumapili kwenye nyumba ambayo alimuelekeza aje kuulizia. Siku ilifika kama walivyoahidiana, masaa machache kabla ya kuwasili Heri alianza kusikia harufu mbaya chumbani kwake, ambayo kwa uzoefu wake aligundua ni ya panya aliyekufa. Akafanya kila kitu ambacho alidhani kinaweza kinaweza kumaliza tatizo kwani muda ulivyozidi kusonga mbele ndiyo harufu nayo ilizidi. Muda wa Nuru kufika ulikaribia. Njia mbadala aliyotumia kuondoa harufu ndiyo iliyoleta balaa zaidi.

# Harufu ya Panya-6

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

UNAWEZA kukaa kitandani hapo? Au nikupishe kwenye kistuli?" Heri akamuuliza.

"Aaa wewe kaa tu kwenye kistuli chako. Mimi nitakaa hata hapa kitandani. Nuru aliamua kukaa kitandani kwa sababu hakukuwa na sehemu nyingine ya kukaa. Hakuwa na kochi zaidi ya kistuli tu ambacho kilikuwa kimekaliwa na mwenyewe.

Hakutaka kumsumbua mwenyeji wake, akaamua tu akae kwenye kitanda ambacho kilikuwa karibu zaidi na mlango.

"Samahani nimekuweka kitandani, maana nyumba yenyewe haina hata kiti, ndiyo tunaanzaanza maisha hivyo."

"Hakuna tabu, siku zote mwanzo mgumu mwaya." Nuru akajibu kumpoza Heri ili kutompa unyonge.

"Hukupotea?" "Hapana, nimekuja kuuliza kumbe nimeshafika. Ile nauliza tu naambiwa nyumba hiyo hapo, ingia kwenye kigeti hicho, nilipoingia nikaona vyumba ya uani na wewe tayari ulishaniambia kuwa chumba chako mtu akiingia kwenye mlango mkubwa kiko upande wa kulia."

"Okay, hata hivyo kichwa chako chepesi sana." Heri akamwambia Nuru na kusababisha aangue kicheko.

Kilichofuata hapo ni mazungumzo ambayo wenyewe watoto wa mjini wanayaita 'arobaini hadithi.'

Ni yale mazungumzo yalisiyokuwa na mada, yanazungumzwa ili mradi muda uende. Kwa sababu hawa walikuwa ndiyo wanataka kuwa wapenzi wapya, ilichukua muda kila mmoja kumzoea mwenzake, hasa kwenye mazungumzo.


Heri, alijikakamua na kumueleza jinsi anavyompenda na angependa awe wake.

"Usinidanganye lakini, maana nyingi wanaume, mhh! Leo unaniambia nakupenda, kesho ukiona sketi nyingine tu mimi huna habari nami tena," alijihami Nuru.

Ukweli ni kwamba kila kitu kiliisha siku ile pale kwenye mgahawa, Chanika madukani.

Siku zote, mwanamke kama hampendi, au hamhitaji mwanaume hawezi kwenda nyumbani kwake hata kwa bahati mbaya.

Yangeishia kule kule, yasingefika huku. Kwa mazungumzo yao yalivyoendelea, tayari kila mmoja alikubali kuingia rasmi kwenye penzi. Baada ya yapo yaliyofuata ni maneno ya kipuuzi yanayofariji. Wenyewe wanayaita maneno ya mapenzi. Kila mmoja alieleza jinsi anavyompenda mwenzake.




**Akamuacha mgeni wake ndani. Akatoka nje na kwenda kuchukua ndoo ya plastiki, akachota maji kutoka kwenye ndoo kubwa zaidi ambayo hutumika kuhifadhia, zamani walikuwa wanaita pipa, lakini siku hizi kwa sababu ni ya plastiki, watayaita jaba.**

Mpaka wakati huo hakuna kilichokamilisha kwa asilimia 100. Ili kukamilisha hilo, Heri alimwambia mpenzi wake mpya kuwa anakwenda kwanza kuoga, halafu akishamaliza ndipo na yeye ampeleke akaoge kwa sababu bafu halijui lilipo.

Akamuacha mgeni wake ndani. Akatoka nje na kwenda kuchukua ndoo ya plastiki, akachota maji kutoka kwenye ndoo kubwa zaidi ambayo hutumika kuhifadhia, zamani walikuwa wanaita pipa, lakini siku hizi kwa sababu ni ya plastiki, watayaita jaba.

Akaingia bafuni kuoga. Alitumia kiasi cha dakika 15 hivi. Aliporidhika kuwa kuwa tayari ameoga inavyotakiwa, alijua kuwa sasa kinachofuata ni zamu ya mpenzi wake Nuru.

Akashuka katika ngazi nne za kutoka bafuni. Akaenda kwenye jaba na kujaza maji mengine ambayo aliyepeleka bafuni.

Kazi iliyobaki sasa ni kwenda kumchukua Nuru ili aje kuoga, kabla ya kupumzika, na baadaye kumrudisha kwao usiku kiasi cha saa mbili au tatu kama alivyojiwekea.

Akafungua mlango ili amchukue mpenzi wake ili kumpeleka bafuni, halafu amuche aoge.

Alimkuta amekaa pale pale kitandani, lakini uso wake ulionekana kuwa umebadilika ghafla na hakuwa na raha au bashasha kama ile ya mwanzo.

"Nuru?" Akaita, lakini hakuitika. Badala yake alikuwa anamtazama kwa namna ya ambayo hata yeye mwenyewe ilianza kumshangaza. Alionekana kuwa na hasira, ambayo kwa kipindi kifupi tu alichotoka kwenda kuoga, hakujua zimekujaje.

Nuru alionekana kuhema kuliko kawaida yake, jambo ambalo lilianza kumtia wasiwasi Heri.

"Kimetokea nini Nuru, mbona uko hivi?" Akauliza tena. Kwa mara nyingine tena hakujibiwa.

Akili ikamwambia labda kuna kitu ambacho amekiona mle ndani hakikumpendeza. Akaenda moja kwa moja kwenye meza yake iliyokuwa imejaa vikorokoro vingi, ikiwemo simu yake ya mkononi.

Akagundua kuwa huenda Nuru amepekuwa simu yake na amekuta meseji ambazo hazikumpendeza.

Akaanza kukumbuka kama baadhi ya meseji zake alizokuwa akichati na msichana aliyemletea supu siku ile aliyokuwa anaumwa kama amezifuta.

Akakumbuka jinsi msichana yule aliyekuwa akisambaza supu ya utumbo ya mama wa jirani, alipomletea, aliomba namba zake za simu akabaki nazo.

Baadaye akaanza kumtumia meseji za kumsifia siku ile alipomletea supu nyumbani jinsi alivyojisikia vizuri. Mara shepu yake na sura zilimchanganya. Meseji ziliendelea kufanya kazi kazi hadi wakawa wapenzi.

Inawezekana wangeendelea kuwa hivyo kama si kurudishwa kwao Lindi ambako ili akaolewe.

Aligundua hilo baada ya wiki mbili za kutomuona na simu yake haikuwa inatumika tena.

Aliogopa kumuuliza mama muuza supu, lakini alipata nyepesi nyepesi dukani kuwa, kilichomponza msichana huyo ambaye alikuja Dar kwa shangazi yake huyo mama Jafari muuza supu kwa ajili ya kumsaidia kazi hizo baada ya kumaliza kidato cha nne.

Kufika Dar, chakula kizuri, nguo za kisasa, huku akimuibia shangazi yake vipodozi anavyoweka kabatini, vilimfanya msichana Sharifa kunawiri, na kupendeza tofauti na ilivyokuwa awali.

Kosa alilolifanya ni kujirekodi kwenye simu ya shangazi yake na kuwapostia ndugu zake Lindi.

Kwa jinsi alipendeza tofauti na alivyokuwa kijijini, iliwapa tamaa ndugu na wazazi kumuozesha.

Baadhi ya vijana wa huko nao alivyokuwa akiona picha za Sharifa, huyu huyu waliyekuwa naye udenda ulianza kuwatoka.

Mmoja wao akaamua kuingia mzima mzima nyumbani kwa wazazi wa Sharifa na kupeleka barua.

Ikakubaliwa, na hapo hapo kijana huyo ambaye alikuwa anazuzuliwa na pesa alizozipata kwa kulima korosho.

Ikapigwa simu haraka kwa shangazi yake kuwa Sharifa anatakiwa arudi nyumbani mama yake mgonjwa.

Aliporudi akaozeshwa fasta, na akabadilishiwa kabisa namba ya simu. Sasa hivi akaishi na mumewe, Mbekenyera. Akaangalia meseji zilizopo hakuona hata moja ambayo ingeweza kumfanya awe katika hali ile inayoonekana kuwa ya hasira ya isiyo ya kawaida.

"Vipi umeletewa taarifa ambayo si nzuri?" Akaendelea kuuliza. Akahisi kuwa huenda amepata meseji au simu ambayo si nzuri. Bado hakujibiwa. Badala yake hali ilionekana kuwa mbaya kwa Nuru.

Alionekana kama mtu aliyefura kwa hasira, lakini pia jasho lilionekana kumtoka licha ya kwamba kulikuwa na feni ilimpepea. Macho yalikuwa yamemtoka pima mithili ya mtu aliyepigwa kabali.

Kila sekunde zilivyozidi kwenda ndiyo hali yake ilizidi kuwa mbaya kiasi cha kumtisha Heri.

Alionekana kama anataka kusema kitu lakini alishindwa. Ni kama kuna kitu kimekaba kooni.

Heri hakuamini alichokiona. Mtu ambaye walikuwa wanaongea na kucheka, amebadilika ghafla.

Aliwahi kusikia hadithi nyingi za wanawake au wanaume wanaofia kwa wapenzi wao. Akaona leo yamemkuta. Alichoona sasa ni kama Nuru anataka kutoka kitandani pale kumvamia, huku akitoa mikoromo ya kutisha.

**ITAENDELEA JUMAPILI**





# SKALES ANATIA HURUMA



MWANAMUZIKI kutoka Nigeria, Skales ameibua hofu kwa mashabiki zake baada ya kueleza anakabiliwa na hali ya upweke.

Kupitia ukurasa wake wa Instagram, Skales kuwa hana mtu wa kumsikiliza, isipokuwa binti yake ambaye alizaa na mkewe wa zamani.

Msanii huyo alieleza kuwa marehemu mama yake alikuwa mwanamke pekee aliyekuwa anamsikiliza na kumuelewa, na kwamba kifo chake kimempa pigo katika maisha yake.

Amesema anahofia maisha yake, yuko katika hali ya upweke uliopita kiasi na hakuna mtu anayependa zaidi moyo wake.

# HAIKUWA RIZIKI

ALIYEKUWA mpenzi wa mwanamuziki maarufu wa Bongo Fleva, Diamond Platnumz, anayefahamika kama Sarah, amesema haikuwa riziki kwake kuwa na msanii huyo katika kipindi cha mafanikio.

Sarah ambaye hivi karibuni amepata umaarufu baada ya mwanamuziki huyo kumpandisha jukwaani na kumshukuru kutokana na wimbo wake 'Kamwambie', amesema Mungu hakupanga kuwa na Diamond na kamwe hawezi kujutia kuachana kutokana na yeye anajiweza kifedha,

"Mimi ni mpambanaji kila kitu kinaenda vizuri, kila kitu kinakuja kama riziki na Mungu hakupanga tuwe pamoja. Diamond na mimi tunaongea na ananipa shukrani nikienda kwenye shoo zake, hivyo hatuna matatizo yoyote," amesema Sarah.

HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### TUCHEL ATAJWA UNITED

KOCHA wa Bayern Munich, Thomas Tuchel, jina lake ni miongoni mwa makocha ambao wako katika orodha ya ya kutakiwa na Manchester United ili kuchukua nafasi ya Erik ten Hag iwapo Mholanzi huyo ataondoka msimu wa joto. (**Times**)

### ARTETA AMTAKA ISAK

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amemfanya mshambuliaji wa Newcastle na Timu ya Taifa ya Sweden, Alexander Isak mwenye miaka 24 kuwa shabaha yake kuu msimu huu wa joto. (**Independent**)

### GABRIEL SAFI ARSENAL

ARSENAL imeanza mazungumzo ya mkataba mpya na mlinzi wa kati wa Brazil, Gabriel mwenye umri wa miaka 26, katika jitihada za kupigana na klabu kubwa za Ulaya. (**Football Insider**)

### ZIRKEE SOKONI ULAYA

MAKAMU wa Rais wa Inter Milan, Javier Zanetti, amependekeza kuwa mabingwa hao wa Serie A huenda wakashindana na Manchester United na Arsenal katika kuinasa saini ya mshambuliaji wa Bologna, Mholanzi Joshua Zirkzee, ambaye ana umri wa miaka 22. (**Mirror**)

### RABIOT ANUKIA UNITED

KLABU ya Manchester United imefanya mawasiliano na wakala wa kiungo wa kati wa kimataifa wa Ufaransa, Adrien Rabiot, mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake na Juventus unakamilika msimu huu wa joto. (**Team Talk**)

### ADARABIOYO KUTUA NEWCASTLE

MLINZI wa kati wa Fulham, Tosin Adarabioyo, mwenye umri wa miaka 26, anaelekea kujiunga na Newcastle baada ya mkataba wake wa sasa utakapokamilika msimu wa joto. (**Mail**)

### EVERTON NA BRANTHWAITE

EVERTON inamatumaini ya kumshawishi, Jarrad Branthwaite, mwenye miaka 21 kusalia Goodison Park kwa mwaka mmoja zaidi lakini Manchester United wana imani dau la pauni milioni 60 waliloweka mezani litakubaliwa. (**Football Insider**)

### SPURS KUMUUZA RICHARLISON

MABOSI wa Tottenham Hotspur watasikiliza ofa kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Richarlison mwenye umri wa miaka 26 msimu huu wa joto. (**Telegraph**)

### MADRID YAMTAKA FRANCO

REAL Madrid imefanya uchunguzi kwa River Plate kuhusu kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Argentina, mwenye umri wa chini ya miaka 20, Franco Mastantuono. (**Fabrizio Romano**)

### PARTEY ATAKIWA BARCA

BARCELONA imemfanya kiungo wa kati wa Arsenal na Timu ya Taifa ya Ghana, Thomas Partey, mwenye miaka 30, kuwa mlengwa wao mkuu katika usajili msimu huu. (**Caught offside**)

### CITY, UNITED VITANI

KLABU ya Manchester City inafikiria kumnunua mlinda mlango wa Lazio, Christos Mandas, huku Manchester United pia ikimtaka mchezaji huyo raia wa Ugiriki mwenye umri wa miaka 22. (**Corriere dello Sport**)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA AFUNGUKA JESUS HAONDOKI

## Asema nyota huyo yuko katika mipango yake licha...

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta, amesema klabu hiyo haina nia ya kumruhusu mshambuliaji wake, Gabriel Jesus kuondoka ifikapo mwisho wa msimu huu.

Ripoti za mapema wiki hii zilidokeza Arsenal itakuwa tayari kusikiliza ofa kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27, ambaye atakuwa amebakiza miaka mitatu katika mkataba wake mwishoni mwa msimu huu.

**Jesus amefunga mabao nane katika mechi 33 msimu huu akicheza kama mshambuliaji wa akiba.**

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil amekuwa na matatizo ya goti tangu afanyiwe upasuaji wa jeraha alilolipata katika Fainali za Kombe la Dunia zilizofanyika Qatar mwaka, 2022.

Alifanyiwa upasuaji mdogo wa pili Januari mwaka huu na alikiri mwezi uliopita "sikumbuki lini nilicheza soka bila maumivu."

Kai Havertz amechukua jukumu muhimu katika kuongoza safu ya ushambuliaji ya Arsenal akichukua nafasi ya Jesus.

Lakini alipoulizwa kuhusu uvumi mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil anaweza kuondoka katika klabu hiyo, Arteta alisema: "Sijui hii inatoka wapi."

Vyanzo vimeambia ESPN, Arsenal iko tayari kuuza wachezaji kadhaa ili kusaidia kuongeza bajeti yao ya uhamisho wa majira ya joto.

Akiulizwa zaidi iwapo alikuwa na nia ya kuruhusu Jesus, ambaye alijiunga na Arsenal kutoka Manchester City kwa pauni milioni 45 mnamo, 2022, aondoke mwishoni mwa kampeni, Arteta alijibu: "Hapana, hapana."

Arteta alisema matumaini yake Jorginho atakubali mkataba mpya hivi karibuni huku mazungumzo yakiendelea.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 unamalizika mwishoni mwa msimu huu na nyota huyo wa kimataifa wa Italia anafikiriwa kutaka kusalia katika klabu hiyo aliyojiunga nayo kutoka Chelsea kwa pauni milioni 12 Januari mwaka jana.

"Ningependa kumbakisha," Arteta alisema. "Anajua hilo. Klabu inaunga mkono kikamilifu hilo. Ni mchezaji muhimu sana kwetu, ndani na nje ya uwanja. Anatufanya kuwa bora zaidi hivyo tunataka abaki."

# SZCZESNY KURUDI LONDON



**LONDON,** England

KLABU ya Chelsea inahusishwa na mpango wa kutaka kumsajili aliyekuwa golikipa wa Arsenal, Wojciech Tomasz Szczesny, itakapofika mwishoni wa msimu huu.

Chelsea wanatajwa wako katika mpango huo, wakiamini Szczesny, anatosha kuwa sehemu ya kikosi ambacho kitaleta mapinduzi msimu ujao wa Ligi Kuu England.

The Blues inadaiwa kutovutiwa na uwezo wa makipa wake wa sasa, Robert Sanchez na Djordje Petrovic, huku Kepa aliopo Real Madrid kwa mkopo, naye anaonekana hatoshi klabuni hapo.

Hata hivyo inadaiwa Juventus inayommiliki kwa sasa, ipo tayari kumwachia mwishoni mwa msimu huu, ikiwa ni mpango wa kutaka kuboresha kikosi chao kwa kuleta changamoto mpya kikosini.

Szczesny ambaye ni raia wa Poland hakuwa na kipindi kizuri zaidi alipokuwa akiitumikia Arsenal.

Arsenal ilikubali kumwachia Szczesny mwaka 2017 baada ya kudumu klabuni hapo kwa miaka nane, akicheza michezo 132.

Akiwa Juventus kuanzia mwaka 2017 amecheza michezo 197, akitwaa mataji Ligi Kuu ya Italia 'Serie A' mara tatu msimu wa 2017-18, 2018-19 na 2019-20.

## Guardiola amtabiria makubwa Phil Foden

**MANCHESTER,** England

PEP Guardiola amesem, Phil Foden atakuwa mmoja wa wachezaji bora kabisa wa Manchester City baada ya kiungo huyo kutangazwa kuwa Mwanasoka Bora wa Mwaka wa Chama cha Waandishi wa Soka (FWA).

Foden alishinda tuzo hiyo baada ya msimu bora zaidi wa maisha yake ya soka ambapo amefunga mabao 24, yakiwamo 16 katika Ligi Kuu England.

Akiwa bado ana umri wa miaka 23 na tayari ameshinda mataji 14 makubwa, Guardiola amesema ataungana na Colin Bell, Mike Summerbee, David Silva na Sergio Agüero kama mmoja wa wachezaji bora katika historia ya klabu hiyo.

"Klabu hii ina historia ndefu, kwa hiyo huwezi kusahau kilichotokea kwa wachezaji waliocheza hapa, kama kila mtu anajua," alisema Guardiola akiwaambia wanahabari jana.

"Nadhani klabu imejengwa na wachezaji wengi wenye ubora wa hali ya juu. Nina hisia kama ataendelea na soka lake hadi mwisho hapa na kuendelea na kiwango hicho anaweza kuwa mmoja wa wachezaji bora, hiyo ni hakika.




"Kwa nini tusisubiri hadi astaafu na baada ya kuona, bado ni mdogo."

Foden jana alitarajiwa kurejea katika kikosi cha City kwa ajili ya mechi ya Ligi Kuu England dhidi ya Wolves iliyotarajiwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Etihad baada ya kukosa ushindi wa 2-0 dhidi ya Nottingham Forest kwa sababu ya ugonjwa.

## Newcastle kumsajili Tosin Adarabioyo

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle United inapewa nafasi kubwa ya kumsajili beki wa Fulham, Tosin Adarabioyo.

Beki huyo amekuwa gumzo katika kipindi baada ya kuonyesha kiwango safi akiwa na Fulham, ambayo hadi sasa imejihakikishia kuwa sehemu ya timu 20 zitakazoshiriki Ligi Kuu England msimu ujao wa mwaka 2024/25.

Newcastle United inatajwa iko katika mpango wa usajili huo, wakizipiku klabu nyingine za England ikiwamo Tottenham na Manchester United huku AC Milan ya Italia ikitajwa pia inahitaji huduma ya nyota huyo.

Mkataba wa beki huyo mwenye umri wa miaka 26 unamalizika mwishoni mwa msimu huu, na tayari ameshathibitisha kutokuwa na mpango wa kuendelea kuitumikia Fulham.

Gazeti la The Sun limeripoti taarifa za Adarabioyo likieleza: "Newcastle wanakaribia kumsajili beki wa Fulham, Tosin Adarabioyo, kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu 2023/24.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 ameripotiwa kupewa ofa ya mkataba wa muda mrefu huko St James' Park wenye thamani ya zaidi ya pauni 100,000 kwa wiki.

Kinda huyo wa zamani wa Manchester City hivi majuzi alisisitiza hamu yake ya kuondoka Fulham msimu wa joto wakati mkataba wake utakapoisha, ambapo SunSport ilifichua hilo tangu Desemba, mwaka jana.

HABARI MICHEZO

# NDUMBARO ANOGESHA BETIKA MBEYA TULIA MARATHON 2024

Na Mwandishi Wetu

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson na Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Dk. Damas Ndumbaro, wamewaongoza mamia ya mashabiki katika 'Amsha Amsha' ya mbio ya Betika Mbeya Tulia Marathoni zilizofanyika Morogoro na jijini, Dodoma jana.

Dk. Tulia aliwaongoza wakimbiaji wa Dodoma wakati Ndumbaro akishiriki mbio za amsha amsha zilizofanyika Morogoro kwa nyakati tofauti huku viongozi hao wakiwasisitiza umuhimu wa kufanya mazoezi na kutumia michezo ikiwamo riadha.

**Mbio hizo ni maalumu maandalizi ya kuelekea kilele cha mbio ya Betika Mbeya Tulia Marathon zitakazofanyika Mei 10 na 11, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Sokoine, Mbeya.**

"Hamasa imekuwa kubwa, kwa namna watu walivyokimbia leo (jana) kule Mbeya patachimbika," alisema Dk. Tulia.

Mbio ya Betika Mbeya Tulia Marathon inayolenga kukusanya fedha kwa ajili ya kuboresha miundo mbinu ya afya na elimu katika jiji la Mbeya na mikoa mingine itashirikisha mbio za marathoni (kilomita 42), nusu marathoni (kilomita 21), kilomita tano na mbio za uwanjani za mita 100, 200, 400 na 1,500.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, atakuwa mgeni rasmi katika mbio hizo.

Ofisa Habari wa Betika, Rugambwa Juvenalius, alisema mbali na amsha amsha iliyofanyika Dodoma, Morogoro, Mtwara leo na kesho mbio hizo zitaendelea katika mikoa ya Rukwa, Iringa na Dar es Salaam.

"Mei 8 itakuwa ni funga kazi ambapo kutakuwa na tukio kubwa pale Mbeya, ikiwa ni maandalizi ya kujiweka tayari kwa msimu wa saba wa mbio hizi," alisema Rugambwa.




Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (katikati mwenye miwani), akiwakabidhi bendera baadhi ya wanariadha walioshiriki mbio za 'Amsha Amsha' zilizofanyika jijini, Dodoma jana kama sehemu ya maandalizi kuelekea msimu wa saba wa Betika Mbeya Tulia Marathon. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simba Queens, JKT kibaruani

Na Saada Akida

VITA ya kuwania umalkia wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania itaendelea tena leo katika viwanja vitano tofauti, mabingwa watetezi, JKT Queens watakuwa ugenini kuwavaa Alliance Girls kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini, Mwanza wakati Simba Queens watawakaribisha Amani Queens.

Mechi nyingine za ligi hiyo itakuwa ni kati ya Bunda Queens dhidi ya Geita Gold Queens itakayochezwa kwenye Uwanja wa Karume mjini Musoma wakati Ceasiaa Girls watakuwa nyumbani dhidi ya Yanga Princess na Fountain Gate Princess watawakaribisha 'majirani' zao Baobab Queens kwenye Uwanja wa Jamhuri.

Simba Queens inaongoza ligi hiyo ikiwa na pointi 37 ikifuatiwa na JKT Queens yenye pointi 28.

Kikosi cha Simba Queens kinahitaji pointi tatu muhimu ili kuendelea kujiimarisha katika vita ya kutwaa taji la ligi hiyo huku JKT Queens wakiendelea kupambana kusaka ushindi na kufufua matumaini ya kulibakisha taji hilo.

Vita nyingine iliyoko katika ligi hiyo ni ya kuwania nafasi ya tatu ambayo inawindwa na Ceasiaa Queens pamoja na Yanga Princess, kila timu ikiwa na pointi 24.

Alliance Girls yenye pointi saba na Geita Gold Queens iliyojikusanyia pointi sita zinaburuza mkia katika ligi hiyo inayoshirikisha timu 10 kutoka mikoa mbalimbali ya Tanzania Bara.

## Simba SC yatamba haiishi mpaka iishe

INATOKA UK. 24

si vinginevyo," alisema Mgunda.

Kuhusu kutoa nafasi kwa wachezaji vijana, Mgunda alisema mchezaji yoyote aliyesajiliwa na Simba lazima anakuwa na uwezo, klabu kama hiyo haiwezi kusajili ili mradi tu, hivyo anatakiwa kuitumikia.

"Katika mechi hii, tulicheza na timu ambayo haijalishi matokeo waliyonayo, ila uwezo waliokuwa nao, wana uwezo mkubwa, wana vijana wazuri wenye vipaji, ila tunashukuru kwa kupata pointi tatu, hii imekwisha tunajipanga na mchezo ujao," Mgunda alisema.

Hata hivyo, Simba inaendelea kushika nafasi ya tatu ikiwa na pointi 50 nyuma ya vinara Yanga yenye pointi 62 na Azam FC yenye alama 54 kibindoni.

Simba itashuka tena dimbani kusaka pointi tatu muhimu za Ligi Kuu Tanzania Bara kesho kwa kuwakaribisha Tabora United na Mei 9, mwaka huu itakutana na Azam FC kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Azam yaifuata Yanga

INATOKA UK. 24

wachezaji wake walionyesha kiwango bora dakika 25 za mwanzo, hata hivyo kipindi cha pili wachezaji wake waliamka na hasa walipofunga goli la nne," alisema Dabo.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema jana mechi zote za hatua ya nusu fainali zitaanza kuchezwa kuanzia saa 9:30 mchana.

"Maandalizi ya mechi zote yanaendelea vyema, tunajua tumefika hatua ngumu ambayo kila timu inahitaji kucheza fainali," alisema Ndimbo

Ihefu yenyewe ilisonga mbele katika mashindano hayo kwa kuifunga Mashujaa FC penalti 4-3 baada ya kutoka suluhu dakika 90 za kawaida huku Coastal Union iliifunga Geita Gold bao 1-0.

Yanga yenyewe ilisonga mbele katika mashindano hayo kwa kuwafunga Tabora United mabao 3-0.

Fainali za mashindano hayo kwa mwaka huu zinatarajia kufanyika kwenye Uwanja wa Tanzanite ulioko Babati mkoani, Manyara.



# Michezo

Jumapili Mei 5, 2024

Nipashe




Arteta afunguka Jesus haondoki UK. 21

# SIMBA SC YATAMBA HAIISHI MPAKA IISHE

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

## Naye winga Karabaka atoa siri baada ya kufunga bao lake la kwanza...

WAKATI uongozi wa Simba ukisema bado hawajakata tamaa ya kukata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao, winga chipukizi wa timu hiyo, Saleh Karabaka, ambaye alifunga bao lake la kwanza juzi amefunguka alichokifanya uwanjani ni 'matunda' kutoka kwa Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mgunda.

Simba ilipata ushindi wake wa kwanza tangu Machi 15, mwaka huu, kwa kuifunga Mtibwa Sugar mabao 2-0, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, shukrani Fred Michael na Karabaka.

Ushindi huo ulianza kufufua matumaini ya Simba kucheza michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika msimu ujao.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema kwa sasa wanaamini watamaliza msimu katika moja kati ya nafasi mbili za juu ili kurejea tena kwenye mashindano ya kimataifa msimu ujao.**

"Kwanza ulikuwa ushindi muhimu ili wachezaji wetu waanze kujisikia vizuri, unajua timu isipopata ushindi, wanaoanza kuathirika ni wachezaji. Pili ni tulikuwa tunahitaji ushindi kwa ajili ya kurudisha imani kwa mashabiki wetu, tatu bado tunasaka nafasi mbili za juu, ubingwa au nafasi ya pili, hatujakata tamaa, tunazidi kupambana, haiishi mpaka iishe," alisema Ahmed.

Nyota wa zamani wa JKU ya Zanzibar, Karabaka, ambaye alifunga bao la pili katika mchezo huo wa juzi alisema kabla ya kuingia uwanjani kama mchezaji wa akiba kipindi cha pili, aliteta na Mgunda.

"Mwalimu (Mgunda), aliniita na kuniambia timu haikimbii, yaani wachezaji wetu wanakwenda langoni kwa wapinzani bila kasi yoyote, akaniambia ili hawa tuwafunge, tuwe tunakimbia muda wote, tukikamata mpira tusiangalie nyuma, sisi ni mbele tu muda wote, nilivyoingia mimi na wachezaji wenzangu wa akiba tukatekeleza majukumu, tukaondoka na ushindi," alisema Karabaka.

Naye Mgunda alisema timu yao bado inaendelea kujipanga kuhakikisha inamaliza msimu kwa kupata matokeo chanya.

"Kwa sasa tunachohitaji ni kushinda michezo yetu, mwisho wa siku ndiyo tutaona tutakuwa tumesimamia wapi, lakini hatujakata tamaa na ubingwa la wala nafasi ya pili, mshindi wa mbio za marathoni anapatikana pale anapogusa na kukata utepe, na

INAENDELEA UK 23



Kiungo mshambuliaji wa Azam FC, Feisal Salum 'Fei Toto' (kulia), akimtoka kipa wa Namungo, Deogratius Munishi 'Dida' katika mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku. Azam ilishinda mabao 4-1. **PICHA: MITANDAO**

# Azam FC yaifuata Yanga FA

**Na Somoe Ng'itu**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Yanga kutoka Dar es Salaam inatarajia kucheza mechi yao ya hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo dhidi ya Ihefu Mei 19, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha, imefahamika.

Nusu fainali nyingine ya mashindano hayo itachezwa Mei 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini, Mwanza kwa kuwakutanisha Azam FC dhidi ya Coastal Union.

Ratiba ya mechi hiyo ilitolewa rasmi jana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), baada ya kukamilika kwa mechi za hatua ya robo fainali ambapo Azam FC ilipata ushindi wa mabao 4-1 dhidi ya Namungo kutoka mkoani Lindi, mechi ikichezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi usiku.

Bao la kwanza la Azam katika mchezo huo lilifungwa na Kipre Junior dakika ya 10 huku Idd Selemani 'Nado' akiandika la pili dakika tano baadaye wakati Feisal Salum 'Fei Toto' yeye alifunga goli dakika ya 19 huku Ayoub Semtawa akipachika bao kwa upande wa wageni dakika chache kabla ya kwenda mapumziko.

Dakika ya 52, Gibril Sillah alifunga bao la nne kwa Azam FC, ikiwa ni siku chache imetoka kuwafunga wenyeji hao wa Ruangwa mabao 2-0, katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Licha ya kupata ushindi huo, Kocha Mkuu wa Azam, Yousuopha Dabo, alisema mechi hiyo haikuwa rahisi kutokana na aina ya wapinzani waliokutana nao.

"Baada ya kupata mabao ya kuongoza, tulionekana kupunguza kasi na kuwapa nafasi wapinzani wetu kupata bao moja. Alisema

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >